Nipashe
Jumatano Julai 22, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580290
The Guardian digital
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



USICHUKULIE POA NYUMBA NI CHOO
Vaa barakoa
USICHUKULIE POA
UNATEGEMEWA

## Makonda atoa neno mchakato wa ubunge Jimbo la Kigamboni

UKURASA 3

KURA ZA MAONI CCM

# VILIO, VICHEKO

**UPEPO** wa Mapinduzi wasomba mawaziri Zanzibar, wabunge maarufu na waliounga juhudi waangukia pua, mawaziri wa JPM wazidi kung'ara... *Endelea uk. 2,3 na 7*

BARA



Askofu Gwajima



David Kafulila



Dk. Harrison Mwakyembe



Kippi Warioba



Prof. Maghembe



Dk. Vicent Mashinji

ZANZIBAR



Mohammed Raza



Dk. Mwinyihaji Makame



Mahmoud Thabit Kombo



Saada Mkuya



Sadifa Juma

## Uchaguzi Mkuu sasa kufanyika Jumatano

UKURASA 3

Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play App Store

MICHEZO YANGA: BIFU BENCHI LA UFUNDI LIPO HAPA UK.24
MAONI, KATUNI UK.6

# Vilio, Vicheko



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango (wa pili kushoto), akiwa na wagombea wenzake kuwania uteuzi wa ubunge wa Jimbo la Buhigwe kwa tiketi ya CCM katika uchaguzi wa kura za maoni uliofanyika jimboni humo, mkoani Kigoma juzi, na kuongoza kwa kupata kura 298. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**Na Waandishi Wetu**

MCHAKATO wa kura za maoni kuomba ridhaa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuteuliwa kuwania nafasi za ubunge na uwakilishi ulihitimishwa jana, huku kukiwa na 'vicheko na vilio' miongoni mwa makada waliokuwa wametia nia.

Matokeo ya kura hizo yameshuhudiwa mawaziri wengi wakifanikiwa kuingia katika hatua ya pili ya mchujo kwa kuongoza katika kura hizo, huku watu mashuhuri akiwamo Askofu wa Kanisa la Ufufuo na Uzima, Josephat Gwajima, wakianguka.

Katika kura hizo, wateuliwa wengi walioamua kuachana na kazi ya utumishi wa umma na kwenda kugombea ubunge, wameanguka, akiwamo aliyewahi kuwa Mbunge wa Kigoma Kusini, David Kafulila, na baadaye kuteuliwa kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Songwe, ameshika nafasi ya nne kwa kupata kura 64.

Aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo, Hasna Mwilima, amepata mwanga wa kutetea nafasi yake baada ya kupata kura 273, akifuatwa na Nashoni Bidyanguze (143) katika nafasi ya pili na January Kizito (118) kwenye nafasi ya tatu.

**KAWE**

Furaha Jacob ameongoza kwa kura 101 akiwazidi makada zaidi ya 100 waliokuwa wamejitokeza kuchukua fomu, akifuatwa na Angellah Kiziga (85) na Askofu Gwajima aliyepigiwa kura 79.

Mbali na watatu hao, jimbo ambalo kwa muda mrefu limekuwa chini ya uwakilishi wa Halima Mdee (CHADEMA), lilimvutia pia aliyekuwa Katibu Mkuu wa CHADEMA, Dk. Vincent Mashinji aliyembulia kura mbili.

**BUCHOSA**

Kwenye Jimbo la Buchosha, wagombea wawili wamefungana kwa nafasi ya kwanza. Wawili hao ni aliyekuwa mbunge wake Dk. Charles Tizeba aliyepata kura 354 na Erick Shigongo aliyepata idadi hiyo ya kura pia huku wagombea wanaowafuatia wakipata kura mbili, moja na wengine kutopata kabisa.

**VWAWA**

Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, ameongoza kwa kura 552 Jimbo la Vwawa, akifuatiwa na Erick Minga (129) katika nafasi ya pili na Dismas Haonga (9) kwenye nafasi ya tatu.

**KASULU MJINI**

Mkoani Kigoma, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, ameongoza kwa kura 405 Jimbo la Kasulu Mjini, akifuatwa na aliyekuwa mbunge wake, Daniel Nsanzugwanko (80) na Thobias Muhanuzi (3).

**MANYOVU**

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, pia ameongoza kwa kura 298 Jimbo la Manyovu, akifuatwa na aliyekuwa mbunge wake, Albert Obama (72) na Abia Nyabakari (26).

**MUHAMBWE**

Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi, Mawasiliano, Atashasta Nditiye, ameongoza kwa kura 212 Jimbo la Muhambwe, akiwazidi kete Jamal Tamimu aliyepata kura 99 na Dickson Bidebeli (50).

**MANONGA**

Wilayani Igunga mkoani Tabora, aliyekuwa Mbunge wa Manonga katika Bunge lililopita, Seif Gulamali ameongoza kwa kura 309, akifuatwa na Abubakar Shaban (227) na Jacob Kwandu (91).

**ILEJE**

Aliyekuwa Mbunge wa Ileje, Janeth Mbene, ameanguka kwa kupata kura 39, akizidiwa na kinara Willium Ndile aliyepigiwa kura 172 akifuatwa na Godfrey Kasekenya (106).

**KONDOA**

Katika Jimbo la Kondoa, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, ameongoza kwa kura 703 akifuatwa na Hassan Lubuva (238) na Issa Orry (36).

**CHEMBA**

Mkoani Dodoma, aliyekuwa Mbunge wa Chemba, Juma Nkamia, ameshika nafasi ya pili kwa kupata kura 162 nyuma ya kinara Mohamed Moni (327) huku Hawa Godwne akikamata nafasi ya tatu kwa kura 68.

**HANDENI VIJIJINI**

Jimbo la Handeni Vijijini, aliyekuwa mbunge wake, Mboni Mhita, ameshika nafasi ya pili kwa kura 136, akizidiwa na Charles Sungura (168) huku nafasi ya tatu ikichukuliwa na Lughenga Abubakar (110).

**NYASSA**

Mkoani Ruvuma, Stella Manyanya, aliyekuwa Mbunge wa Nyasa na Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara ameibuka kidedea kwenye jimbo hilo.

**TUNDURU KUSINI**

Katika Jimbo la Tunduru Kusini, aliyekuwa mbunge wake, Daimu Mpakate ameibuka mshindi kwa kupata kura 582, akifuatwa na Mtutula Abdallah (143) na Mtamila Achikuo (22).

**MTWARA MJINI**

Mkoani Mtwara, Jimbo la Mtwara Mjini ambalo Bunge lililopita lilikuwa chini ya uwakilishi wa Maftaha Nachuma (CUF), Judith Nguli ameng'ara kwa kura 126, akifuatwa na Hassan Mtenga (94) na aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Newala, Mussa Chima (86).

**IRAMBA MAGHARIBI**

Mkoani Singida, Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Mwigulu Nchemba, ameongoza kwa kura 677, nafasi ya pili ikichukuliwa na Jumbe Katalah (14) na Noel Kingu aliyeshika nafasi ya tatu kwa kura sita (6) kusaka kuteuliwa kuwania Jimbo la Iramba Magharibi.

**IRAMBA MASHARIKI**

Wakati hali ikiwa hivyo Iramba Magharibi, Jimbo la Iramba Mashariki ameongoza Fransis Isack kwa kura 209, akifuatwa na Emmanuel Mkumbo (161), huku aliyekuwa mbunge wake, Allan Kiulah akianguka baada ya kupata kura 159.

**SUMVE**

Mkoani Mwanza, Kasalali Mganga ameongoza kwa kura 138 Jimbo la Sumve, akifuatwa na Bulaga (131) na Busigasolwe Shinje (110).

**NYAMAGANA**

Stanslaus Mabula ameongoza kwa kura 319 Jimbo la Nyamagana jijini Mwanza aliokuwa mbunge wake kwa miaka mitano tangu 2015, akifuatwa na John Nzilanyingi (54) na John Nzwalile (46).

**UKEREWE**

Jimbo la Ukerewe nafasi ya kwanza imechukuliwa na Joseph Mkundi kwa kura 171, akifuatwa na Babilasi (108) na Kasiri (95).

**MBINGA VIJIJINI**

Jimbo la Mbinga Vijijini lilikuwa na mchuano mkali kati ya Benaya Kapinga aliyeongoza kwa kura 247 na Gaudencia Kayombo aliyepigiwa kura 196.

**SONGEA MJINI**

Mkoani Ruvuma, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Damas Ndumbaro, ameongoza kwa kura 315 akifuatwa na Jeremia (34) katika kusaka kuteuliwa na CCM kuwania ubunge wa Songea Mjini.

**MULEBA KUSINI**

Katika Jimbo la Muleba Kusini, aliyekuwa mbunge wake na Waziri wa zamani wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Charles Mwijage, ameng'ara kwa kura 387, akifuatwa na Edward Mjungu (135) na Adorian Bitegeko (30).

**KARAGWE**

Waziri wa Viwanda na Biashara, ameanza safari ya kutetea ubunge wa Karagwe baada ya kupata kura 587, akiwaacha kwa mbali Joseph Kahama (48) na Lameck Byamukama (6).

**BUKONA MJINI**

Katika Jimbo la Bukoba Mjini ambalo Bunge lililopita lilikuwa chini ya uwakilishi wa Wilfred Lwakatare (CHADEMA), nafasi ya kwanza imechukuliwa na Almasud Kalumuna aliyepata kura 116, akifuatwa na Muhaji Kachwamba (36) na Anatory Amani (17).

**NAMTUMBO**

Kwenye Jimbo la Namtumbo, aliyekuwa mbunge wake, Edwin Ngonyani, ameongoza kwa kura 188, akifuatwa na Vita Kawawa aliyepata kura 163 na Mussa Chowo (122).

**BUYUNGU**

Mkoani Kigoma, Aloyce Kamamba, ameongoza kwa kura 50 dhidi ya 47 za Msakila Kabende 44 za Emmanuel Gwegenyeza katika kinyang'anyiro cha kusaka kuteuliwa kuwania Jimbo la Buyungu.

**KIGOMA MJINI**

Vilevile, katika Jimbo la Kigoma Mjini ambalo kwenye Bunge lililopita lilikuwa chini ya Zitto Kabwe (ACT-Wazalendo), Kilumbe Ngenda ameongozwa kwa kura 218, akifuatwa na Juma Juma (44) na James Nyabakari (37).

Wakati hali ikiwa hivyo mjini Kigoma, katika Jimbo la Kasulu Vijijini, Augustino Vuma ameng'ara kwa kura 266, akifuatwa na Agripina Buyogera (97) na Samweli Kadogo (70).

**MASASI MJINI**

Geoffrey Mwambe, aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji (TIC), ameongoza kwa kura 337, akimwangusha aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo, Rashid Chuachua, aliyepigiwa kura 127.

**KIGOMA KASKAZINI**

Kwenye Jimbo la Kigoma Kaskazini, aliyekuwa mbunge wake na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Peter Serukamba, ameongoza kwa kura 261 akifuatwa na Assa Makanika (81) na Suleiman Mvunye (51).

**SHINYANGA MJINI**

Mkoani Shinyanga kumeshuhudiwa aliyekuwa Mbunge wa Shinyanga Mjini, Steven Masele, akiendelea kung'ara baada ya kupata kura 152 akifuatwa na Jonathan Manya (65) na Gasper Kileo (51), huku aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini, Patrobas Katambi, akipata kura 120.

**SOLWA**

Shinyanga Vijijini kulikuwa na mchuano mkali kati ya aliyekuwa Mbunge wa Solwa katika Bunge lililopita, Ahmed Salum, na aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Shinyanga Azza Hamad.

Hata hivyo, Salum aliibuka kinara baada ya kupata kura 377 dhidi ya 304 za Hamad na 35 za Jeremiah Jiriri aliyeshika nafasi ya tatu.

**KISHAPU**

Wilayani Kishapu mkoani Shinyanga, Suleiman Nchambi, aliyekuwa Mbunge wa Kishapu katika Bunge la 11, ameongoza kwa kura 544, akifuatwa na Kishiwa Kapale (54) na Boniphace Butondo (40).

## Uchaguzi Mkuu sasa kufanyika Jumatano

**Na Romana Mallya**

KWA mara ya kwanza uchaguzi mkuu wa urais, makamu wa rais, ubunge na udiwani utafanyika Jumatano badala ya Jumapili kama ilivyozoeleka.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, (NEC), Jaji wa Rufani mstaafu, Semistocles Kaijage, alisema uchaguzi mkuu wa mwaka huu unatarajia kufanyika Oktoba 28.

Akitangaza ratiba ya uchaguzi, Jaji mstaafu, Kaijage alisema Agosti 25, kutafanyika uteuzi wa wagombea kiti cha urais, makamu wa rais, ubunge na udiwani na Agosti 26 kampeni za uchaguzi zitaanza hadi Oktoba 27.

Ingawa Jaji Kaijage, hakutoa ufafanuzi kuhusiana na uamuzi wa uchaguzi mkuu kufanyika Jumatano, lakini kumekuwapo na mapendekezo kutoka kwa wadau wa uchaguzi na makundi mengine ya jamii nchini kutaka uchaguzi huo kutofanyika Jumapili kama ilivyokuwa kwa miaka yote.

Wamekuwa wakisema kuwa watu wengi wamekuwa wakipata wakati mgumu kwenda kupiga kura Jumapili sambamba na kuhudhuria ibada makanisani.

## Makonda awashukuru wakazi wa Kigamboni

**Na Mary Geofrey**

ALIYEKUWA Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, amewashukuru wananchi wa Kigamboni kwa matokeo aliyopata katika kura za maoni za Chama Cha Mapinduzi (CCM) za kuwania ubunge wa Jimbo la Kigamboni.

Makonda alitoa pongezi hizo jana ikiwa ni siku moja baada ya kushika nafasi ya pili katika kura hizo zilizofanyika juzi jijini Dar es Salaam.

Makonda alikuwa miongoni mwa wagombea 78 waliotia nia ya kuomba ridhaa ya CCM kumpitisha kuwania ubunge wa jimbo hilo, akiwamo mbunge anayemaliza muda wake, Dk. Faustine Ndugulile, aliyeongoza katika kura hizo.

Makonda alitoa shukrani hizo jana kupitia ukurasa wake wa Instagram, kufuatia kura 122 dhidi ya Dk. Ndugulile aliyepata kura 190.

"Nimepata pole nyingi sana kutokana na matokeo ya jana. Kwanza nawashukuru kwa upendo wenu na maombi yenu ya kunitakia mafanikio katika kutimiza ndoto yangu," alisema Makonda.

"Jambo moja Kubwa na muhimu ni kuyajua mapenzi ya Mungu na katika hili mapenzi ya Mungu ni makubwa kuliko mapenzi yangu. Nawatakia baraka na afya njema siku zote za maisha yenu."

"Asanteni sana sana wana Kigamboni kwa upendo wenu na kunipa nafasi niwe sehemu ya maisha yenu."

# Upepo wa Mapinduzi wasomba mawaziri Zanzibar

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MAWAZIRI watatu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na vigogo waliogombea nafasi ya uwakilishi wameangushwa katika kura za maoni.

Kadhalika, vigogo wengine kadhaa wamedondoka katika kuwania ubunge na uwakilishi.

Baadhi ya mawaziri hao ni wa Katiba na Sheria, Khamis Juma Mwalimu, Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale, Mahmoud Thabit Kombo na Waziri wa Kilimo Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Mmanga Mjengo Mjawari.

Khamis Juma Mwalimu aligombea Jimbo la Pangawe nafasi ya uwakilishi na alipata kura 53 dhidi ya mpinzani wake, Ali Suleiman Ameir Mrembo, ambaye alipata kura 57.

Mahmoud Thabit Kombo aliyegombea Jimbo la Kiembe Samaki nafasi ya uwakilishi aliangushwa baada ya kupata kura 30 dhidi ya mpinzani wake, Suleiman Haroub Suleiman, ambaye alipata kura 52.

Kwa upande wake Mmanga Mjengo Mjawiri ambaye aligombea nafasi ya urais wa Zanzibar, lakini hakufanikiwa kuchaguliwa pia ameangushwa katika kura ya maoni kwa kupata kura 52 ambapo Abdallah Hussein Kombo alipata kura 57.

Pia wapo wanasiasa wakongwe walioangushwa akiwamo mbunge aliyemaliza muda wake, Sadifa Juma ambaye aliwania uwakilishi katika Jimbo la Donge, ambalo alikuwa analiongoza kama mbunge kabla ya kujitosa kwenye uwakilishi.

Yumo pia Dk. Mwinyihaji Makame aliyeogombea uwakilishi Jimbo la Dimani na Rashid Ali Juma ambaye aligombea uwakilishi wa Jimbo la Amani. Radhid Ali Juma pia alikuwa mtiania wa urais wa Zanzibar kupitia CCM, lakini jina lake halikupitishwa.

Dk. Mwinyihaji ambae anatetea tena nafasi yake katika jimbo hilo, alipata kura 29 na Mwanaasha Khamis alipata kura 52.

Katika orodha ya waliodondoka yumo pia mfanyabiashara maarufu Mohammed Raza katika kura za maoni Jimbo la Uzini nafasi ya uwakilishi na Sada Mkuya uwakilishi Jimbo la Kikwajuni.

**WALIOONGOZA**

Katika hatua nyingine, wawakilishi na wabunge wanaotetea nafasi zao ambao wamepata nafasi ya kwanza katika kura hizo ni Mwakilishi wa Jimbo la Makunduchi, Haroun Ali Suleiman ambae pia ni waziri wa utumishi wa umma na utawala bora.

Issa Gavu ameongoza katika nafasi ya uwakilishi wa Jimbo la Chwaka. Gavu pia ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Baraza la Mapinduzi.

Wengine ni Haji Omar Kheir uwakilishi jimbo la Tumbatu. Kheir pia ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ pamoja na Juma Makungu Juma aliyeongoza nafasi ya uwakilishi Jimbo la Kijini. Makungu kadhalika ni Naibu Waziri wa Ardhi, Makazi,Maji na Nishati.

Wengine ni Hamad Yussuf Masauni aliyeongoza ubunge Jimbo la Kikwajuni, Simai Mohammed Said uwakilishi Jimbo la Tunguu, Jaku Hashim Ayoub uwakilishi Jimbo la Paje, Hamza Hassan Juma uwakilishi jimbo la Shauri Moyo na Salum Pondeza ubunge Jimbo la Chumbuni.

Vile vile Mohammed Said Dimwa uwakilishi Jimbo la Mpendae na Salim Turkey ubunge Jimbo la Mpendae, Hussein Ibrahim Makungu uwakilishi Jimbo la Mtoni na Nadrir Abdul latif Yussuf uwakilishi Jimbo la Chaani.

Hata hivyo, katika mchakato huo wa kura za maoni, wanawake hawakupata nafasi kubwa. Waliongoza katika majimbo matano tu kati ya majimbo 32.

# Waliohamia CCM waanguka

■ Mwakyembe, Maghembe

**Na Waandishi Wetu**

MAKADA wa vyama vya upinzani waliojiunga na Chama Cha Mapinduzi (CCM) na kutaka kutetea nafasi ya ubunge katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu, wamefanya vibaya kwenye kura za maoni za chama hicho.

Katika kura hizo zilizoanza juzi na kuhitimishwa jana, kumeshuhudiwa pia baadhi ya makada wakongwe wa CCM na mawaziri wakianguka.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Godwin Mollel, ndiye pekee aliyekuwa ameona mwanga wa kutetea jimbo lake kati ya waliokuwa wabunge wa Bunge la 11 waliotoka upinzani na kujiunga na CCM, kwa matokeo ambayo yalikuwa yametufikia hadi tunaingia mtamboni.

Dk. Mollel alimshinda kwa kura moja aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, katika kinyang'anyiro cha kusaka kuteuliwa kuwania Jimbo la Siha mkoani Kilimanjaro.



**TANDAHIMBA**

Aliyekuwa Mbunge wa Tandahimba kupitia Chama cha Wananchi (CUF) na baadaye kujiunga na Chama Cha Mapinduzi (CCM), Katani Katani, ameshika nafasi ya pili akipigiwa kura 308 dhidi ya kura 324 za Dk. Twahili Salum.

Wakati hali ikiwa hivyo kwa makada hao wapya wa CCM, mkoani Mbeya, aliyekuwa Mbunge wa Kyela na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, ameshika nafasi ya tatu kwa kupata kura 252, akizidiwa na Ally Mlagila, maarufu Kinanasi aliyepata kura 502 huku nafasi ya pili ikichukuliwa na Hunter Mwakifuna (288).

**MWANGA**

Katika Jimbo la Mwanga mkoani Kilimanjaro, aliyekuwa mbunge wake, Profesa Jumanne Maghembe, ameanguka kwenye kura hizo za maoni, akishika nafasi ya pili kwa kupata kura 130, nyuma ya kinara Anania Thadayo (176) huku nafasi ya tatu ikishikwa na Shabibu Mruma (56).

MVOMERO

Naibu Waziri wa zamani katika wizara zinazohusika na habari na maji, Amos Makala, ameongoza kwa kura 321 katika Jimbo la Mvomero alilowahi kuwa mbunge wake kwenye Bunge la 10, akifuatwa na aliyekuwa mbunge wake Bunge lililopita, Selemani Sadiq 231 na Jonas Van Zeland (112).

**KAHAMA**

Mjini Kahama, aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo Jumanne Kishimba ameongoza kwa kura 234, akifuatiwa na Benjamini Ngaiwa (181) na James Lembeli (54).

**MSALALA**

Jimbo la Msalala, aliyekuwa mbunge wake Ezekiel Maige ameshika nafasi ya pili kwa kura 118, akizidiwa na Idd Khassim (327).

# Majambazi yavunja maduka yapora mamilioni ya shilingi

**Na Gaudence Msuya, KIBITI**

WATU wanaosadikiwa kuwa majambazi, wamevamia maduka matano mji mdogo wa Mjawa Magharibi likiwamo la wakala wa fedha na kupora jumla ya Sh. milioni 21.

Kwa mujibu wa habari zilizopatikana na kuthibitishwa na Kamanda wa Polisi wa Kanda Maalumu ya kipolisi ya Rifiji, Onesmo Lyanga, uvamizi huo ulifanyika saa 8.00 usiku wa kuamkia juzi katika Kijiji cha Mjawa Magharibi, Kata ya Mjawa, wilayani Kibiti.

Watu waliozungumza na mwandishi wa habari hizi kuhusiana na tukio hilo walisema walipoamka asubuhi walikuta maduka hayo yanayomilikiwa na wafanyabiashara wakubwa ndiyo yaliyoporwa.

Mmoja wa wafanyabiashara waliovunjiwa, Shaaban Matandiko, alisema amerudishwa nyuma na kuviomba vyombo vya ulinzi na usalama kuchunguza walihusika na tukio hilo.

"Tunaogopa hata kufanya biashara sasa kwa sababu tunahofu huenda wakarudi tena au wakapora maduka mengine, tegemeo letu ni vyombo vya dola kufanya uchunguzi na kisha kuwanasa waliohusika," alisema Shaaban.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Mjawa Magharibi, Mohamed Jongo, alisema hilo ni tukio la pili kufanyika kijijini hapo, la kwanza likuwa la majambazi kumkata mwananchi kwa mapanga.

Alisema serikali ya kijiji hicho imeshawasiliana na vyombo vya dola ili vipeleke wataalamu watakaobaini wahusika na kwamba kwenye duka la fedha la M-Pesa jumla ya Sh. milioni nne ziliporwa.

Akithibitisha habari hizi, Kamanda Onesmo alisema watu kadhaa wanashikiliwa kuhusiana na tukio hilo, wakiwamo walinzi wa maduka hayo na kwamba uchunguzi zaidi unafanyika ili kuwanasa waliohusika ujambazi huo.

"Kwa sasa siwezi kuzungumzia lolote kuhusiana na tukio hilo kwa sababu tayari maofisa wa jeshi hilo wapo katika uchunguzi...tuna uhakika kwamba tutawanasa wote na watafikishwa kwenye vyombo vya serikali," alisema Onesmo.

# Canara Bank (Tanzania) Ltd.

(Together we can build a better life)

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 JUNI 2020

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | Robo Mwaka ya sasa 30 Juni 2020 | Robo Mwaka iliopita 31 Machi 2020 |
|---|---|---|---|
| A | **MALI** | | |
| | 1 Fedha Taslimu | 868.48 | 796.63 |
| | 2 Salio katika Benki kuu ya Tanzania | 9,141.69 | 17,653.40 |
| | 3 Uwekezaji katika Amana za serikali | 27,017.89 | 18,619.79 |
| | 4 Salio katika Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 623.14 | 777.39 |
| | 5 Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 108.86 | 61.95 |
| | 6 Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| | 7 Bili zilizoafikiwa | - | - |
| | 8 Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| | 9 Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 33,767.13 | 30,836.28 |
| | 10 Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| | 11 Mikopo Halisi Iliyopo | 36,268.16 | 38,521.20 |
| | 12 Mali Nyingine | 850.70 | 857.05 |
| | 13 Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| | 14 Akaunti za udhamini | - | - |
| | 15 Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,350.25 | 1,452.86 |
| | **16 JUMLA YA MALI** | **109,996.28** | **109,576.53** |
| B | **DHIMA** | | |
| | 17 Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 26,845.00 | 29,050.00 |
| | 18 Amana za Wateja | 44,206.80 | 42,081.30 |
| | 19 Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | 20 Amana Maalumu | - | - |
| | 21 Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| | 22 Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| | 23 Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,310.63 | 1,137.08 |
| | 24 Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| | 25 Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| | 26 Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| | 27 Dhima Nyingine | 673.95 | 819.25 |
| | 28 Madeni | - | - |
| | **29 JUMLA YA DHIMA** | **73,036.38** | **73,087.63** |
| | **30 MALI/(DHIMA) HALISI** *(16 kutoa 29* | **36,959.90** | **36,488.90** |
| C | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| | 31 Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 32,830.00 | 32,830.00 |
| | 32 Akiba ya Mtaji | 880.66 | 788.02 |
| | 33 Mapato Yaliyobakizwa | 2,256.62 | 2,349.26 |
| | 34 Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 992.62 | 521.62 |
| | 35 Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| | 36 Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| | **37 JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **36,959.90** | **36,488.90** |
| | 38 Dhima Zisizo Dhahiri | 16,878.33 | 14,538.72 |
| | 39 Mikopo Chechefu | 4,219.68 | 4,032.28 |
| | 40 Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 110.72 | 282.27 |
| | 41 Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| | (i) Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 33.60% | 33.30% |
| | (ii) Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 11.60% | 10.42% |
| | (iii) Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 51.18% | 54.41% |
| | (iv) Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 32.97% | 35.15% |
| | (v) Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 88.80% | 81.00% |
| | (vi) Ongezeko la Amana | -0.11% | 1.76% |
| | (vii) Ongezeko la Mali | 0.38% | 1.45% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 JUNI 2020

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo Mwaka ya sasa 30 Juni 2020 | Robo ya mwaka linganishi (mwaka uliopita) 30 Juni 2019 | Limbikizo la mwaka wa sasa 30Juni 2020 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 30 Juni 2019 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 2,076.28 | 1,980.91 | 4,204.70 | 3,817.06 |
| 2 Gharama za Riba | 789.45 | 652.09 | 1,571.07 | 1,193.13 |
| **3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **1,286.83** | **1,328.82** | **2,633.63** | **2,623.93** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (171.55) | 60.00 | (52.18) | 120.00 |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba** | **147.48** | **300.55** | **339.50** | **495.63** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 60.31 | 35.50 | 96.24 | 86.68 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 87.16 | 265.05 | 243.26 | 408.95 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | - | - | - | - |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **984.85** | **1,029.77** | **1,672.69** | **2,088.53** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 325.61 | 408.39 | 645.76 | 745.66 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 4.57 | 8.48 | 9.35 | 13.11 |
| 7.3 Gharama Nyingine | 654.67 | 612.90 | 1,017.58 | 1,329.76 |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **621.00** | **539.60** | **1,352.62** | **911.03** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 150.00 | 160.00 | 360.00 | 280.00 |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **471.00** | **379.60** | **992.62** | **631.03** |
| 11 Idadi ya Waajiriwa | 25 | 25 | 25 | 25 |
| 12 Mapato kwa Hisa | 14 | 12 | 30 | 19 |
| 13 Mapato kwa Hisa | 14 | 12 | 30 | 19 |
| **14 Idadi ya Matawi** | 1 | 1 | 1 | 1 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (I) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1.75% | 1.54% | 1.84% | 2.56% |
| (II) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 5.13% | 4.35% | 5.44% | 7.22% |
| (III) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 68.66% | 63.20% | 56.26% | 66.95% |
| (IV) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 5.40% | 5.97% | 5.51% | 7.37% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 JUNI 2020

*(Kiasi kwa shilingi milioni )*

| | | Robo Mwaka ya sasa 30 Juni 2020 | Robo Mwaka iliopita 31 Machi 2020 | Limbikizo la mwaka wa sasa 30 Juni 2020 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 30 Juni 2019 |
|---|---|---|---|---|---|
| I | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 471.00 | 521.62 | 992.62 | 631.03 |
| | Marekebisho kwa ajili ya: | - | - | - | - |
| | Hasara katika mali | 107.35 | 111.70 | 219.06 | 480.00 |
| | -Badiliko halisi katika Mikopo | 2,253.04 | (2,887.18) | (634.15) | 245.33 |
| | Faida/Hasara kwenye mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | Mabadiliko halisi katika Amana | (79.50) | 1,231.84 | 1,152.34 | (4,855.88) |
| | Mabadiliko halisi katika Amana za muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | Mabadiliko halisi katika dhima nyingine | 234.96 | 98.60 | 333.55 | 606.95 |
| | Mabadiliko Halisi katika mali nyingine | (2,688.16) | 1,217.81 | (1,470.35) | 216.16 |
| | Kodi iliyolipwa | (150.00) | (210.00) | (360.00) | - |
| | Mengineyo(bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **148.68** | **84.39** | **233.07** | **(2,676.41)** |
| II | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za kudumu | (4.74) | (8.38) | (13.12) | (9.54) |
| | Mapato kutokana na mauzo ya mali za kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana zilizoshughulikiwa na Mawakala | (15,011.15) | 5,611.17 | (9,399.98) | (8,090.02) |
| | Mapato kutokana na mauzo ya Amana zilizoshugulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo(bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uwekezaji** | **(15,015.89)** | **5,602.79** | **(9,413.10)** | **(8,099.56)** |
| III | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato kutokana na utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko halisi katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo(bainisha) | (56.83) | (74.57) | (131.40) | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za kifedha** | **(56.83)** | **(74.57)** | **(131.40)** | **-** |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha taslimu** | | | | |
| | Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (14,924.04) | 5,612.61 | (9,311.43) | (10,775.97) |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo mwaka/mwaka | 53,982.48 | 48,369.87 | 48,369.87 | 42,092.56 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo mwaka/mwaka** | **39,058.44** | **53,982.48** | **39,058.44** | **31,316.59** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 Juni 2020

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Tengo la Ziada ya jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Robo Mwaka wa sasa 30/06/2020** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa Robo mwaka** | **32,830.00** | - | **2,870.88** | **788.02** | - | - | **36,488.90** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 471.00 | - | - | - | **471.00** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (92.65) | 92.65 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa Robo mwaka wa sasa** | **32,830.00** | - | **3,249.23** | **880.66** | - | - | **36,959.90** |
| **Mwaka Uliopita 31/12/2019** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka Uliopita** | **32,830.00** | - | **2,308.69** | **828.58** | - | - | **35,967.28** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 521.62 | - | - | - | **521.62** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 40.56 | (40.56) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka Uliopita** | **32,830.00** | - | **2,870.88** | **788.02** | - | - | **36,488.90** |

**BAADHI YA MAELEZO**
**KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI 2020**

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha,sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita(kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka sasa,mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| Jina | Cheo | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| T R BALAJI RAO | OFISA MTENDAJI MKUU | (Imesainiwa) | 17-07-2020 |
| FADHILI PETRO SANGA | MKUU WA FEDHA | (Imesainiwa) | 17-07-2020 |
| FREDRICK HIPPOLITE | MKAGUZI MKUU WA NDANI | (Imesainiwa) | 17-07-2020 |

**Sisi tuliotajwa hapo chini wajumbe wa bodi ya wakurugenzi tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu,tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na zinaonesha hali halisi..**

| Jina | Cheo | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| 1. RAJABU SELEMANI KAKUSA | MKURUGENZI | (Imesainiwa) | 17-07-2020 |
| 2. INDIAEL DANIEL KAAYA | MKURUGENZI | (Imesainiwa) | 17-07-2020 |

Canara Bank (T) Ltd
Head Office Dar Es Salaam Branch
Elia Complex P.O. Box 491, Dar Es Salaam, Tanzania
E:mail ctbl@canarabank.co.tz, T +255 222112530 (D) +255 222112532
www.canarabank.co.tz

215819802

# Sababu wanawake kuanguka ni hizi

**Na Romana Mallya**

WADAU wamepongeza mwamko wa wanawake katika kinyang'anyiko ya uchaguzi majimboni huku wakilalamikia mfumo dume kuwaangusha kwenye mchakato wa kura za maoni mwaka huu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, akitoa maoni yake kuhusu idadi ndogo ya wanawake waliopita katika mchakato wa kura za maoni, alisema bado kuna tatizo.

"Nilifurahi kuona katika uchaguzi huu wanawake wengi wamejitokeza kugombea nafasi mbalimbali ikiwamo ubunge ingawa waliopita ni wachache na sura zilizopitishwa ni zilezile," alisema.

Henga alisema bado kuna mfumo dume katika jamii kuwa mwanamke hawezi kuongoza kama ilivyo kwa wanaume na hata akiongoza hawezi kuwa kiongozi mzuri.

"Wapiga kura nao ni sehemu ya jamii hiyo hiyo ambayo inaamini mwanaume ndiye mwenye uwezo wa kuongoza kuliko mwanamke, hivyo bado ipo kazi kubwa ya kutoa elimu hususani kwenye vyama ili mabadiliko yaanzie huko," alisema.

Mchambuzi na mtetezi wa haki za wanawake, Dk. Ananilea Nkya, alisema wameshuhudia kuwapo kwa watia nia wengi wanawake mwaka huu na kuripotiwa tatizo la rushwa baadhi ya maeneo.

"Kama rushwa imetembea unategemea ni watiania wangapi wanawake wanaweza kutembeza rushwa ili wapate nafasi.

"TAKUKURU (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa) kila wakati imekuwa ikisema kuna rushwa hapa mara pale na wanawake wengi hawapo tayari kujihusisha na rushwa na kama wapo ni wachache."

# HELSB yaanza rasmi kupokea maombi mikopo elimu ya juu

**Na Ismail Ngayonga**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) jana imetangaza kuanza kupokea maombi ya mikopo kwa njia ya mtandao kwa mwaka wa masomo 2020/2021 kuanzia Julai 12 hadi Agosti 31, 2020.

Akizungumza na wanahabari katika ofisi za HESLB jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji, Abdul-Razaq Badru, amesema waombaji wote wa mkopo wanashauriwa kusoma na kuuzingatia 'Mwongozo wa Utoaji Mikopo kwa 2020-2021' unaopatikana katika tovuti ya HESLB (www.heslb.go.tz). "Mwombaji anaweza kuingia kwenye mfumo wetu kupitia tovuti yetu ambayo ni www.heslb.go.tz na atapata maelekezo ya kutosha ya kuingia katika mfumo wa OLAS – Online Loan Application System," alisema Badru.

Kuhusu bajeti ya fedha za mikopo, alisema serikali imetenga Sh. bilioni 464 kwa mwaka 2020/2021 ambazo zinatarajia kuwanufaisha jumla ya wanafunzi 145,000. Kati yao 54,000, watakua ni mwaka wa kwanza na wengine 91,000 ni wanaoendelea na masomo.

**BAJETI 2020-2021**

"Bajeti hii ya Sh. bilioni 464 kwa 2020/2021 imeongezeka kutoka Sh. bilioni 450 mwaka 2019/2020 ambazo zinawanufaisha jumla ya wanafunzi 132,119," alisema Badru wakati akiwafafanulia mwanahabari.

Kuhusu wanafunzi wahitaji wa mkopo waliomaliza kidato cha sita na wanaotarajia kujiunga kambi ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), alisema utaratibu wa kuwafikia unaandaliwa.

"Tunafahamu kuwa kuna wanafunzi waliomaliza kidato cha sita wanaotarajia kujiunga na kambi 18 za Jeshi la Kujenga Taifa kuanzia mwezi Agosti, 2020, tunakamilisha utaratibu kwa kushauriana na Makao Makuu ya JKT ili kuwawezesha wakati huo," alisema.

**MALIPO CHAKULA NA MALAZI**

Akitoa ufafanuzi kuhusu malipo ya robo ya nne ya fedha za chakula na malazi kwa wanafunzi waliopo vyuoni hivi sasa, alisema HESLB inakamilisha malipo hayo kwa wanafunzi 132,119 ambao wanaufaika hivi sasa.

"Tumeanza kulipa na tunakamilisha malipo hayo ambayo hulipwa kwa mwanafunzi mnufaika moja kwa moja ili kumuwezesha kumudu gharama za chakula na malazi katika siku zote anazokuwa chuoni kama tunavyoelezwa na chuo husika," alisema na kuongeza:

"Ufafanuzi huu tunautoa kwa kuwa tumepokea maoni kutoka baadhi ya wateja wetu ambao ni wanafunzi hawajaelewa vizuri utaratibu huu wa malipo haya na ada za mafunzo ambazo hulipwa mara mbili kwa mwaka."

**MAMBO YA KUZINGATIA**

Ofisa Mikopo Mwandamizi wa HESLB, Josephat Bwathondi, amewakumbusha waombaji kuhakikisha wanafuata maelekezo ikiwamo kutumia namba moja ya kidato cha nne katika kuomba mkopo na kuomba udahili chuoni.

Kwa mujibu wa Bwathondi, uzoefu wa uchambuzi wa maombi ya mikopo umeonyesha kuwa baadhi ya waombaji hukosea kwa kuambatanisha nyaraka zisizotambulika na hivyo kukosa mkopo na kushindwa kutimiza ndoto zao.


## Canara Bank (Tanzania) Ltd.

(Together we can build a better life)

**DISCLOSURE UNDER REGULATION 12 OF BANKING & FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATIONS 2014**

**CUSTOMER COMPLAINT REDRESSAL MECHANISM: To The Esteemed Customers Canara Bank (Tanzania) Ltd Tanzania**

**1. INTRODUCTION (UTANGULIZI)**

The Complaints Resolution Desk (the Desk) has been established by the Bank of Tanzania (BOT) as a cost effective and efficient mechanism to resolve complaints between banking institutions and their customers. The Desk, which is fully funded by the Bank, is intended to resolve complaints (small claims) whose monetary value in respect of both the claim amount and remedy awarded does not exceed fifteen million Tanzania shillings (15,000,000) Mn.

**2. HOW TO LODGE A COMPLAINT WITH OUR BANK (JINSI YA KUWASILISHA MALALAMIKO KWA DAWATI)**

When you are dissatisfied with our services or you have any complaint pertaining to our staff or bank or otherwise, you may lodge complaint to us in writing by post or fax or through your registered email address on the following contact addresses.

**General Manager (Operations) Canara Bank (Tanzania) Ltd,**
**Dar es Salaam Branch,**
**Post Box 491 Dar es Salaam**
**Phone : +255 (22) 2112532**
**Fax: +255 (22)2112534**
**E Mail : cbtl@canarabank.co.tz**

**The Nodal Officer, Grievance Redressal Cell,**
**Canara Bank (Tanzania) Ltd**
**Post Box 491 Dar es Salaam,**
**Phone : +255 (22) 2112530;**
**Fax: +255 (22)2112534**
**E Mail compliance.cbtl@canarabank.co.tz**

**NOTE:**
- For lodging complaint with BOT please use Complaint Form No 1.
- For detailed information for lodging compliant with BOT please visit BOT website https://www.bot-tz.org.

**3. INTERNAL COMPLIANT RESLUTION MECHANISM (MCHAKATO WA KUTAFUTA UFUMBUZI WA MALALAMIKO)**

We through our internal complaint handling mechanism shall resolve your complaints within 21 working days from the date of lodging the compliant. The Internal Complaint handling mechanism in our Bank is as under:
- Receiving and timely processing consumers' complaints.
- Keeping complainants updated throughout the process.
- Keeping a record of all complaints and submit it to the Bank of Tanzania on quarterly basis.
- Resolving all consumer complaints within 21 working days from the date of lodging the complaint.
- In exceptional circumstances if we are unable to resolve the complaint within 21 working days, we will immediately inform the complainant of our inability and reason for the inability and what measures are being taken to resolve the matter urgently and in any case not more than 14 working days thereafter.

**4. HOW TO LODGE A COMPLAINT WITH THE DESK AT BANK OF TANZANIA (BOT) (NAMNA YA KUWASILISHA LALAMIKO KWA DAWATI LA BOT)**

If you are dissatisfied with the decision of our Bank in respect of your compliant or do not receive a response from our Bank within 21 working days from the date of lodging your complaint, you may within 14 working days lodge your complaint with the Desk at BOT. However, before lodging your complaint with the Desk at BOT, you are required to exhaust the Internal Complaints resolution mechanism of our Bank first.

The compliant with Complaints Resolution Desk at Bank of Tanzania shall be lodged in the prescribed form (Schedule A), duly signed by the complainant and shall be submitted in any of the following ways:
a) By hand or by post to:
Complaint Resolution Desk
Office of the Secretary to the Bank of Tanzania,
10 Mirambo Street,
11884, Dar es Salaam.
b) By electronic mail: complaints-desk@bot.go.tz
d) By facsimile to fax no: +255 22 2234067
e) By phone: +255 22 2233265/ +255 22 2233246

**Note:**
a) Complaints shall be lodged with the Desk from 9.00 AM to 12.30 Pm (Monday to Friday).
b) Your complaint must be lodged before expiry of two years after the cause of action arose.

**5. PECUNIARY JURISDICTION OF THE BOT DESK (MAMLAKA ZA KIFEDHA ZA DAWATI)**

The desk shall handle complaints whose total monetary value in respect of both the claim amount and remedy to be awarded does not exceed Fifteen Million Tanzania Shillings (TZS 15,000,000/-).

**6. ELIGIBLE COMPLAINTS (MALALAMIKO YA HAKI)**

Only the following categories of complaints are eligible for submission to the Desk;
a) A complaint against a banking institution which is either a member of the Tanzania Bankers Association or regulated by the Bank.
b) A complaint which is lodged within 14 days after a banking institution has delivered its decision or has failed to respond.
c) A complaint in respect of an incident which occurred less than two (2) years ago.

**7. INELIGIBLE COMPLAINTS (MALALAMIKO YASIYO NA HAKI)**

In terms of the Guidelines issued, the Desk considers the following complaints as ineligible:
a) A complaint which has been the subject of legal proceedings before a Court or Tribunal.
b) Where the complainant has not suffered any financial loss, material inconvenience or distress.
c) A complaint which would be more suitably dealt with by a Court or under other dispute resolution arrangement.
d) A complaint whose resolution would prejudice the rights of other parties who have not consented to the resolution by the Desk.
e) A complaint which is vexatious or frivolous or not in good faith.
f) A complaint which was not first reported to the banking institution concerned.
g) A complaint which is lodged more than 14 days after a banking institution has delivered its decision or failed to resolve the complaint.
h) A complaint which is beyond the pecuniary jurisdiction of the Desk.

**8. INFORMATION YOU MUST INCLUDE IN THE COMPLAINT (TAARIFA MUHIMU ZA KUJUMUISHA KWENYE LALAMIKO)**
a) Your name and address.
b) The name and address of the banking institution against which the complaint is made.
c) Details of what your complaint is about including exactly what the bank did that it shouldn't have done or what it didn't do that it should have done.
d) What you have lost in terms of personal injustice, financial loss, hardship or inconvenience.
e) What you would like the Desk to do to put things right and details of what you have done so far to try to resolve the complaint
f) Include documentary evidence, if any.

**9. WITHDRAWAL OF THE COMPLAINT (KUFUTA LALAMIKO)**

A complainant may, at any time before the Desk's determination, withdraw his complaint in writing from the Desk, and the matter shall be closed by the Desk.

**10. FREE SERVICE (HUDUMA ZA BURE)**

Resolution of banking consumers' complaints is free of charge as the Desk does not charge any fee whatsoever.

**11. MEDIUM OF COMMUNICATION (NJIA YA MAWASILIANO)**

The medium of communication is both English and Kiswahili.

**12. REMEDIES AWARDED (SULUHISHO LILILOPATIKANA)**

The function performed by the Desk is different from that performed by courts. The Desk is enjoined not to have regard to technicality and legal form but resolve complaints using criteria that would not usually be used by courts; for instance whether an explanation for the conduct was not given when it should have been given. A banking institution may be required to issue an apology, change its practices, effect payment or compensation as the case may be. The Desk is not bound by the legal principles of handling complaints such as rules of evidence but adheres to the general principles of natural justice.

When Aggrieved by Desk decision

Either party may request the Desk to reconsider any of its decision. Each party also has a right to seek redress before a competent court when it is not satisfied with the decision given by the Desk

**CANARA BANK (TANZANIA) LIMITED**
**SERVICES CHARG**

| | TZS | USD |
|---|---|---|
| **A. SAVINGS BANK** | | |
| 1. Monthly Maintanance Charges | FREE | FREE |
| 2. Non Maintanance of Minimum Balance | FREE | FREE |
| 3. A/C Statement Charges | | |
| a) Monthly | FREE | FREE |
| b) Interm | 5,000.00 | $5 |
| 4. Cash Withdrawl Charges | FREE | Upto 5000 Free Above 5000 - 0.3% |
| 5. Cash Deposit Charges | FREE | FREE |
| 6. Balance Confirmation certificate | 15,000.00 | $7 |
| 7. A/c Closure charges | 15,000.00 | $15 |
| 8. Activation of Dormat A/c | 6,000.00 | $6 |
| **B. CURRENT ACCOUNT** | | |
| 1. Monthly Maintanance Charges | FREE | FREE |
| 2. Non Maintanance of Minimum Balance | FREE | FREE |
| 3. A/C Statement Charges a) Monthly b) Interm | **5000 5000+500 for each page** | **$5 $ 5+1 for each page** |
| 4. Cash Withdrawl Charges | UPTO 25 MIO- FREE ABOVE 25 MIO--0.12% | Upto 5000 Free 5000 to 10,000 - 0.3% Above 10,000 - 0.5% |
| 5. Cash Deposit Charges | UPTO 50 MIO- FREE ABOVE 50 MIO--0.12% | **Upto 10,000- Free > 10,000- 0.3%** |
| 5. Balance Confirmation certificate | 25,000.00 | $15 |
| 6. Stop Payment Charges | 30,000.00 | $15 |
| 7. Cheque Return Charges | | |
| a) Inward | 30,000.00 | $15 |
| b) Outward | 30,000.00 | $20 |
| 8. A/c closure charges | 25,000.00 | $20 |

| **D. REMITTANCES** | | |
|---|---|---|
| | TZS | USD |
| 1. TISS | 11,800.00 | $11.8 |
| 2. E Remittances | | |
| Upto USD 1000 or Eq. TZS | 20,000.00 | $10 |
| 1001 to 5000 | 24,000.00 | $12 |
| 5001 to 10000 | 48,000.00 | $25 |
| 10,001 and above | 100,000.00 | $50 |
| 3. SWIFT | | |
| a) Swift Outward | | |
| Upto 5,000 | NA | $45 |
| 5,001 to 10,000 | NA | $60 |
| above 10,000 | NA | $90 |
| b) Swift Inward | | |
| Upto 5,000 | NA | $12 |
| 5,001 to 10,000 | NA | $18 |
| above 10,000 | NA | $30 |
| **E. LOAN/ADVANCES RELATED CHARGES** | | |
| 1. Processing Charges | Upto 5 Mio - 25,000 5Mio to 10 Mio - 200,000 10 Mio to 25mio - 400,000 25 mn to 500 mio - 1.5% >500mio--1.25%* *minimum 7.5mio | Upto 5,000 - $100 5000 to 10,000 - $200 Upto 20,000 - $300 20,000 to 500,000 - 1.5% >500,000--1.25%* *minimum 7,500 |
| 2. Documentation Charges | Upto 100 mio --NIL-- >100 Mio 0.3% -Min 300,000 | Upto 50,000 --NIL-- >50,000 - 0.3% Min 150 |
| 3. Upfront fee on Term Loan | Upto 5Mio - 25,000 5 Mio to 10 Mio - 200,000 10Mio 25mio - 450,000 25 mn to 500 mio -1.8% >500mio--1.5%* *minimum 9mio | Upto 20,000 - $300 20,000 to 500,000 - 1.8% >500,000--1.5%* *minimum 9000 |
| 4. Inspection Charges | Upto 100 Mio -25,000 >100 mio - 50,000 | Upto 50,000 - 25 >50,000 ----50 |
| **F. LETTER OF CREDIT** | | |
| **Import Letter of Credit (per qrtr of Part thereof)** | | |
| Opening commission | NA | 1.2% ( Min $ 200) |
| LC amendment Commission | NA | 0.4% ( Min $50 max 350) |
| Swift charge for LC opening | NA | $40 |
| Swift charge for other message/amendments | NA | $40 |
| Extensions - Commissions | NA | 1.2% ( Min $200) |
| LC cancellation charges | NA | 1.2% ( Min $200) |
| Non payment of Bills on due date | NA | 16% Till Payment |
| **Export Letters of Credit (per quarter or part thereof)** | | |
| Advising commission | NA | $140 |
| Confirmation Commission | NA | 0.5% ( Min $150) |
| Negotiating bills under LC | NA | 0.5%(Min $75+cuourier+int) |
| Reimbursement claim paid | NA | 0.5% ( Min$75) |
| Extensions - Commissions | NA | 1.2% ( Min $200) |
| Collection of Export LC | NA | 0.5%(Min $75+cuourier+int) |
| Amendments | NA | $75 |
| **G. Guarantees (Local & International)** | | |
| Bonds & Guarantees | 1.2% ( Min TZS 75,000) | 1.20% |
| Bonds & Guarantees with 100 % Cash Margin | 0.5% per quarter (Min TZS 75,000) | 40% of actual charges |

| **C. MOBILE BANKING CHARGES** | | |
|---|---|---|
| 1. Cash Withdrawal | | |
| Upto 100,000 | 2,000.00 | NA |
| 101,000 to 200,000 | 3,000.00 | NA |
| 201,000 to 400,000 | 5,000.00 | NA |
| 401,000 to 600,000 | 6,000.00 | NA |
| 601,000 to 999,000 | 8,000.00 | NA |
| 2. Funds Transfer/Mobile Wallet | | |
| Upto 100,000 | 500.00 | NA |
| 101,000 to 250,000 | 1,000.00 | NA |
| 251,000 to 500,000 | 2,000.00 | NA |
| 501,000 to 1,000,000 | 5,000.00 | NA |
| 1,001,000 TO 10 Mn | 10,000.00 | NA |
| | | |
| Mobile Banking Services | | |
| A) Monthly Subscription Charges | 500.00 | NA |
| B) PIN Request | 2,500.00 | NA |
| **H. LOCKERS RENT YEARLY** | | |
| 1.SMALL | 350,000.00 | |
| 2. MEDIUM | 600,000.00 | |
| 3. BIG | 750,000.00 | |

**OTHER DISCLOSURES(VIAMBATANISHI)**

| | TZS | USD |
|---|---|---|
| 1. Base or Prime Lending Rate | 16 | 7 |
| 2. Maximum spread above Base or Prime Lending Rate | 4 | 4 |
| 3.Penal Interest | | |
| a. For non compliance on Terms of Saction | 3% p.a over regular rate of interest | |
| b. For Overdrawing/Excess drawing due to non payment of interest/installment/charges | 5% p.a over regular rate of interest | |
| 4. Deposit Rates | | |
| a. Current account | Nill | Nill |
| b. Savings bank deposit | 2.50% | 0.50% |
| c. Fixed deposits | | |

i. Fixed Deposits of TZS

| Amount in TZS | up to TZS 10 Million | TZS 10 to 100 Million | Above TZS 100 Million |
|---|---|---|---|
| 31-90days | 3.50% | 4.50% | 5% |
| 91-180days | 4.50% | 5% | 5% |
| 181-364 days | 6% | 6.50% | 6.50% |
| 1-2years | 7% | 7.50% | 8% |
| Over 2 years | 8% | 8.50% | 9% |

ii. Fixed Deposits of USD

| Amount in USD | up to USD 5000 | USD 5000-50,000 | Over USD 50,000 |
|---|---|---|---|
| 31-90days | 0.50% | 1% | 1.50% |
| 91-180days | 1% | 2% | 2.25% |
| 181-364 days | 2% | 2.25% | 2.75% |
| 1-2years | 2.25% | 2.75% | 3% |
| Over 2 years | 2.50% | 3% | 3.50% |

2158198O2

**Banking Services offered BY Canara Bank (Tanzania) Ltd** **We offer following Services**

- Current and Saving Account
- Salary Account
- Student Account
- Fixed Deposit Account
- Re Investment Deposit Account
- Recurring Deposit Account
- Overdraft and Term Loans
- Vehicle Loan
- Mortgage Loan
- Personal Loan
- Insurance Premium Funding
- Safe Deposit Lockers
- All Export and Import Related transactions
- Letter of Credit and Guarantees
- E- Remit Facility to India
- Mobile Banking

Plot No 16/1, Elia Complex
Zanaki-Bibi Titi Street, P.O.Box 491- Dar es Salaam, Tanzania
T: +255 222 112 2530 (D) +255 222 112 532
Email: cbtl@canarabank.co.tz

Access your A/c 24x7

# HABARI PICHANI



Kada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Hadija Kusaga, akijinadi kwa wajumbe wa mkutano mkuu wa Jimbo la Ukonga, ili wamchague katika kura za maoni za kugombea ubunge wa jimbo hilo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Baadhi ya wagombea nafasi ya kuteuliwa kuwania ubunge wa Jimbo la Kawe kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), wakiwa katika uchaguzi wa kura za maoni jimboni humo, Manispaa ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Wajumbe wakipiga kura ya maoni kumchagua mgombea nafasi ya kuteuliwa kuwania ubunge wa Jimbo la Kawe, kwa tiketi ya CCM, katika uchaguzi uliofanyika jimboni humo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Wasimamizi wa uchaguzi wa kura za maoni za ubunge wa Jimbo la Muheza, mkoani Tanga, wakiwa makini kufuatilia uchaguzi huo, mbele ya wajumbe wa mkutano mkuu wa CCM Wilaya ya Muheza jana. Kutoka (kushoto) ni Mwenyekiti wa CCM wilaya, Laick Gugu, Katibu wa CCM wa wilaya hiyo, Mohamed Moyo na mwandishi wa zoezi hilo, kutoka ofisi ya chama hicho, Beatrice Zongwe. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Baadhi ya wana CCM waliochukua fomu za kugombea ubunge katika Jimbo la Babati Mjini mkoani Manyara waliopo viti vya mbele wakisubiri kupigiwa kura na wajumbe wa mkutano mkuu wa wilaya jana. **PICHA: GIFT THADEY**



Aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Bumbuli Wilaya ya Lushoto Mkoa wa Tanga, January Makamba, akiwaonyesha sanduku la kura wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), baada ya kutangazwa mshindi wa kura za maoni kuwania ubunge wa jimbo hilo. Makamba alipata kura 680 dhidi ya Abdulkadir Mghen aliyepata kura 21. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

# Ajali ya magari matatu, bajaji yaua na kujeruhi

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

MTU mmoja amefariki dunia papo hapo na wengine watatu kujeruhiwa baada ya lori la mizigo lililokuwa limesheheni mbolea, kufeli breki na kuyaparamia magari matatu na bajaji moja kwenye mteremko wa Mlima Mbalizi mkoani Mbeya.

Ajali hiyo ilitokea jana saa 4:30 asubuhi ambapo lori lenye namba za usajili T. 952 DJZ na tela lenye namba za T. 277 BNN aina ya Howo lililokuwa linatokea Mbeya Mjini kuelekea katika Mji wa Tunduma mkoani Songwe, liliyagonga magari madogo mawili na lori moja ambayo namba zake hazikujulikana.

Aidha, lori hilo liliigonga bajaji yenye namba za usajili MC- 671 CMX aina ya TVS ambayo ilikuwa imembeba mwanamke mmoja asiyefahamika jina wala makazi yake ambaye alifariki papo hapo.

Kaimu Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Sebastian Mbuta, alisema mwili wa aliyafariki umehifadhiwa katika Hospitali Teule ya Wilaya ya Mbeya Ifisi, na kwamba majeruhi wanaendelea na matibabu katika hospitali hiyo.

"Tulianzisha utaratibu wa magari makubwa na madogo kupita katika mlima huo na milima mingine kwa awamu ili kuepuka madhara kama haya, lakini kilichotokea ni hawa wenye magari madogo waliokaidi kusimama wakati ilikuwa ni zamu ya magari makubwa," alisema Kamanda Mbuta.

Alisema kati ya magari yaliyohusika kwenye ajali hiyo moja ni ya Serikali ambayo imeharibika vibaya na kwamba hata bajaji iliyogongwa ilikiuka utaratibu wa kupita kwa awamu.

Kamanda Mbuta alitoa wito kwa watumiaji wa vyombo vya moto mkoani humo kuendelea kufuata sheria za usalama barabarani ikiwamo kupita kwa awamu kwenye maeneo ya miteremko.

Baadhi ya mashuhuda wa ajali hiyo ambao walikuwa kwenye moja ya magari yaliyoparamiwa na roli hilo, walisema waliliona likiwa linashuka kwa kasi katika mteremko huo ndipo wakaanza juhudi za kulikwepa, lakini likawagusa.

Mmoja wa mashuhuda hao, Abdinasir Mohamed, ambaye ni miongoni mwa madereva, alisema baada ya kuliona lori hilo alilikwepa, lakini kutokana na mazingira ya barabara hiyo alishindwa kulikwepa vizuri ndipo gari lake likakwaruzwa nyuma.

"Nisingelikwepa haraka tulikuwa tunaelekea kugongana uso kwa uso, lakini baada ya kuliona nililikwepa na kabla sijamaliza kukwepa likanikwaruza nyuma na kutoa tairi moja," alisema Mohamed.

Alisema baada ya kulikwepa ndipo lilipoanza kuyaparamia magari mengine ambayo yalikuwa yanashuka ikiwamo bajaji ambayo mwanamke aliyefariki alikuwa amepanda.

Hata hivyo, Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji kikiongozwa na Stafu Sajenti, Hafidh Makumila, kilifika katika eneo la tukio na kuwasaidia kuwaokoa majeruhi na kuwakimbiza katika Hospitali Teule ya Ifisi.

Mbali na kufanya uokozi, pia kikosi hicho kilifanya usafi wa barabara hiyo kwa kuondoa mafuta yaliyokuwa yamemwagika kwa ajili ya kuruhusu magari kuendelea kuitumia bila kupata madhara.



Wakazi wa Mji wa Mbalizi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wakishuhudia ajali ya magari matatu na bajaji moja iliyotokea katika mteremko wa Mlima Mbalizi jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Marufuku sherehe za kuongoza kura za maoni

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

WANAOGOMBEA uteuzi wa nafasi ya ubunge Jimbo la Shinyanga Mjini kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), wamepigwa marufuku kusherehekea kura walizozipata, na watakaofanya hivyo watakuwa wamekiuka maagizo ya chama na watachukuliwa hatua.

Imeelezwa kuongoza kwenye kura za maoni siyo kwamba mhusika umeteuliwa na CCM kupeperusha bendera ya chama hicho kwenye uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu, bali hiyo ni hatua ya awali ambapo majina ya wagombea yatapelekwa kwenye vikao vya Taifa vya chama hicho kupitisha jina la mgombea mmoja.

Hayo yalibainishwa juzi na msimamizi wa uchaguzi wa kura za maoni za ubunge Jimbo la Shinyanga Mjini, Joachim Simbila, baada ya kumaliza kutangaza matokeo ya kura za maoni.

Alisema maelekezo ya chama ni marufuku mgombea aliyeongoza kura za maoni kufanya sherehe za aina yoyote, kwa kuwa haijulikani kama jina lake litakuwa limepitishwa kwa ajili ya kupeperusha bendera ya CCM wakati wa uchaguzi mkuu.

"Marufuku wagombea waliooongoza kwenye kura za maoni kufanya sherehe za aina yoyote ile, bali wasubiri hadi pale tutakaposhinda kwenye uchaguzi mkuu ndipo tutafanya sherehe, lakini kwa sasa hakuna kufanya hivyo," alisema Simbila.

# Waliojimilikisha mali za kanisa wapewa angalizo

**Na Frank Kaundula, MOROGORO**

KATIBU Mkuu Kiongozi wa Kanisa la Afrika Inland Church Tanzania (AIC) wilayani Mvomero, Mchungaji Josephales Mtebe, amesema kanisa lake litawachukulia hatua za kinidhamu wachungaji na waumini wanaodaiwa kijimilikisha mali za kanisa.

Katibu huyo aliyasema hayo juzi kwenye kikao cha kujadili masuala mbalimbali yanayohusu maendeleo ya Dayosisi za kanisa hilo Kanda ya Pwani pamoja kumuaga Askofu wa Dayosisi ya Pwani Charles Salala.

"Kuna baadhi ya wachungaji na waumini wa kanisa hili wanatuhumiwa kijimilikisha mali za kanisa kinyume cha utaratibu, uchunguzi unafanya ili hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yao ili kuwapa fundisho," alisema Mchungaji Mtebe.

Alisema kitendo cha kijimilikisha mali za kanisa bila idhini ni kosa kubwa, na kwamba hakitoi picha nzuri kwa waumini wengine, hivyo wote wanaohusika na tuhuma hizo ni lazima wachukuliwe hatua zinazostahili ili liwe funzo kwao.

Alisema kuwa mbali na kuhubiri mafundisho ya Mungu yatokanayo na Biblia, pia kanisa limekuwa likitoa michango mbalimbali kwa vituo vya kulelea watoto wanaoishi katika mazingira magumu wilayani Mvomero.

Alisema kanisani limekuwa likipokea misaada kutoka kwa wafadhili mbalimbali kwa ndani na nje ya nchi, ambao nao huipeleka kwa watu wenye mahitaji wakiwamo watoto yatima, hivyo kitendo kilichofanywa na wachungaji hao ni cha aibu kubwa.

Aidha, aliwataka waumini wake kuendelea kuvuta subira wakati utaratibu wa kuwashughulikia wote wanaodaiwa kulihujumu kanisa hilo ukiandaliwa.

"Tuendelee kumtegemea Mungu kwani ndiye muweza wa yote, huu siyo muda wa kulaumiana, kunyosheana vidole kwani utaratibu unaandaliwa ili huwashughulikia wanaolihujumu kanisa, hivyo tunakiwa kuliombea kanisa letu," alisema Mchungaji Mtebe.

Naye Katibu wa Kanda ya Pwani, Mchungaji Emmanuel Masanja, alitoa wito kwa waumini kujitokeza kushiriki kikamilifu katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28, mwaka huu ili kuwapata viongozi bora.

Mchungaji Masanja aliwataka waumini wa kaniasa hilo washiriki kikamilifu katika kuliombea taifa pamoja na uchaguzi mkuu ili ufanyike kwa amani na viongozi bora wapatikane.

HABARI KITAIFA

# Sekta binafsi kuwaunganisha wadau wake nchi nzima

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), imewahakikishia wanachama wake wote kuwa itaendelea kuwa kiungo muhimu kwa wadau wote ikiwemo sekta ya umma sambamba na kufanikisha mageuzi ya kiuchumi na kijamii yanayoendelea nchini.

Hayo yalibainishwa na Mwenyekiti wa taasisi hiyo, Angelina Ngalula na kwamba TPSF ipo imara na itaendelea kushirikiana na serikali katika kuwaletea Watanzania maendeleo ya kiuchumi.

"TPSF chini ya Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Zachy Mbenna kwa pamoja tutaendelea kufanyia kazi masuala yote yalipelekea kuundwa kwa TPSF. Kumekuwa na ushirikiano mkubwa kati yetu na serikali," alisema.

Ngalula alisema taasisi hiyo itaendelea kutumia fursa zote ambazo zinapatikana ndani na nje ya nchi na kuwafanya wadau wake wazidi kunufaika kwa kutanua masoko la bidhaa zinazozalishwa na wadau wake, kuhamasisha na kukuza uwekezaji hapa nchini.

"Mkakati wetu kwa sasa ni kutanua huduma zetu nje ya mipaka ya Tanzania na kuimarisha masoko ya ndani, ushiriki wa ujenzi wa miundombinu pamoja na kuendelea kufanya uwekezaji kwenye miundombinu iliyo tayari," alisema Ngalula.

Aidha, aliwasihi wadau wa TPSF kuzidi kuungana hasa katika kipindi hiki ambacho taasisi hiyo imefanya mabadiliko ya kiuongozi baada ya aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo Godfrey Simbeye kumaliza muda wake.

"Kama sekta binafsi tupo imara na mikakati yetu nikufikia malengo ya kuleta mabadiliko katika nyanja ya uchumi na jamiii," alisema Ngalula na kuwataka wanachama na wadau wote kuzitumia fursa mbalimbali za kiuchumi na kibiashara kubadilisha maisha.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo, Mbenna alisema ataitumia nafasi hiyo kuwaunganisha wadau wote na kuzidi kupanua majukumu ya taasisi kimataifa,.

"Ni wakati wa kuzidi kuwaleta pamoja wadau wa sekta binafsi na sekta ya umma ili kwa pamoja tuweze kusukuma maendeleo ya nchi yetu," alisema Mbenna na kuongeza kuwa lengo la taasisi hiyo ni kuwatumikia wadau wote kwa kiwango cha juu cha utoaji wa huduma katika sekta zote," alisema.

# NARCO yamsimamisha meneja tuhuma za upotevu ng'ombe 32

**Na Mwandishi Wetu,**

KAIMU Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Ranchi ya Taifa (NARCO), Masele Mipawa, amemsimamisha kazi Meneja wa Ranchi ya West Kilimanjaro iliyopo Arusha, Hezron Kyaruzi, kwa tuhuma za kukosa uadilifu kwa mali za umma na kusababisha upotevu wa ng'ombe takriban 32.

Akiwa katika ziara ya kutembelea Ranchi hiyo mwishoni mwa wiki, Mipawa alisema kuwa waliamua kufanya uamuzi huo kufuatia changamoto nyingi zinazoikumba shamba hilo ambazo kwa kiasi kikubwa zimechangiwa na uongozi mbovu wa meneja huyo.

"Kutokana na upotevu wa ng'ombe, uzembe na ukosefu wa maadili tumeamua kumsimamisha kazi Meneja wa Ranchi na msaidizi wake na hatua nyingine za kisheria na kinidhamu zitafuata," alisema Mipawa.

**Ziara hii imetusaidia kubaini kuwa kuna wizi uliokithiri katika shamba hili ambao umechangiwa na uhusiano mbovu kati ya meneja na jamii inayozunguka shamba hili.**

Mipawa alisema ziara hiyo aliyoifanya katika Ranchi hiyo ni kufanya ukaguzi kutokana na taarifa walizokuwa wakizipata ambazo zilionesha kuwa katika shamba hilo kumetokea upotevu wa ng'ombe ambao NARCO haina taarifa nao.

"Ziara hii imetusaidia kubaini kuwa kuna wizi uliokithiri katika shamba hili ambao umechangiwa na mahusiano mabovu kati ya meneja na jamii inayozunguka shamba hili, ukosefu wa maadili na uadilifu wa Meneja ambao umepelekea ng'ombe 32 kupotea," alisema.

"Kati ya ng'ombe hao 32 walipotea 15 wameshapatikana na wengine 17 hawajapatikana mpaka sasa huku ng'ombe wengine 27 walichinjwa bila kibali cha makao makuu," alifafanua Mipawa.

Kufuatia hali hiyo, Mipawa alisema wameamua pia kumsimamisha kazi msaidizi wake kwa kuwa alishindwa kumshauri vizuri meneja huyo, huku ikidaiwa alikuwa akishirikiana na meneja huyo kwenda kuazima ng'ombe kwa watu binafsi ili ranchi hiyo ionekane ina idadi kubwa ya ng'ombe.

Aidha, Mipawa aliwataka wafanyakazi wengine waliobaki katika shamba hilo kuendelea kufanya kazi kwa bidii, wazingatie nidhamu na uzalendo huku akiwaonya kuwa Serikali ya haitavumilia mtu yeyote anayehujumu rasilimali za Taifa.




Mafundi wakiendelea na ujenzi wa daraja litakalounganisha eneo la Ubungo na kituo cha daladala cha Mawasiliano, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wawezeshaji waandaliwa uhakiki kaya maskini

**Na Happy Severine,** BARIADI

MKURUGENZI Mtendaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Ladislaus Mwamanga, amewataka wawezeshaji na wakuu wa idara wilayani Bariadi mkoani Simiyu kuwa na kushirikiana katika kusimamia uhakiki wa kaya maskini ili kufuata kanuni na kuzingatia sheria zilizowekwa katika kuzibaini kaya hizo.

Wito huo aliutoa jana wakati wa mafunzo ya kuwajengea uelewa wakuu wa idara na wawezeshaji wa TASAF ngazi ya Halmashauri kufanya kazi kwa uaminifu na uadilifu ili kutimiza adhma ya serikali ya kuwahudumia wananchi.

Mkurugenzi huyo alisema wawezeshaji na wakuu wa idara wanaoshiriki mafunzo hayo kuwa wasikivu ili ujuzi watakaoupata ukawasaidie kufanikisha malengo ya Serikali.

"Niwaombe ndugu zangu mnaopata mafunzo haya kujifunza kwa umakini mkubwa na kwenda kutumia ujuzi mtakaoupata hapa kwa weledi na uaminifu mkubwa mkiweka mbele maslahi ya Taifa na huduma kwa wananchi wetu," Mwamanga.

Mwawanga alisema mafunzo hayo yamelenga kuwaongezea ujuzi wataalamu (wawezeshaji) katika kutambua na kutoa taarifa sahihi za wanufaika wa miradi ya TASAF katika Halmashauri.

Alisema kutambua walengwa kunafanyika kwa maagizo ya Rais John Magufuli alipozindua awamu ya pili ya Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini, huku akibainisha kuwa kumekuwa na taarifa za malalamiko kuwa wapo wanufaika ambao hawastahili kunufaika na mpango huo wakiwapo wenye uhitaji ambao hawajapata nafasi kwenye mpango huo.

Aliongeza kuwa kwa kipindi cha pili cha awamu ya tatu ya TASAF inategemea kuzifanyia uhakiki kaya 4110 huku akibainisha kuwa awamu hii imeweka mkazo kwa kaya kufanya kazi ili kuongeza kipato.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Bariadi, Melckzedeck Humble, alimhakikishia Mkurugenzi wa TASAF kuwa watahakikisha walengwa wote wanafikiwa na kuwaondoa wale wasio na sifa katika mpango huo.

Mratibu wa TASAF wa Halmashauri ya Mji wa Bariadi, Issa Mtweve, alisema awamu iliyopita walikumbana na changamoto kadhaa lakini kwa sasa wamejipanga kufanya uhakiki ulio sahihi ili wanufaika wawe ni wale wenye sifa zinazohitajika.

John Mogela mwezeshaji kutoka Kara ya Malambo Mjini Bariadi, alisema watatekeleza maagizo waliyopewa na kufuata kanuni zilizopo wakati wa uhakiki wa kaya hizo bila kujali kiongozi wa chama fulani wala nyadhifa ya mtu.

# RC atoa onyo kwa wakulima wa bangi Mlali Mvomero

**NA Frank Kaundula,** MOROGORO

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Loata Ole Sanare, ametoa onyo kali kwa wakazi wa Mlali wilayani Mvomero kuacha tabia ya kulima na kuuza madawa ya kulevya aina ya bangi ambapo amesema yeyote atayekutwa nayo hataonewa huruma.

Ole Sanare alitoa onyo hilo jana baada ya kubaini kuwa wakazi wa Kata ya Mlali wengi wengi wao wanajihusisha na kilimo cha zao haramu la mbagi lakini pia wamekuwa wakiiuza hadharani kana kwamba serikali yote ni mali yao.

"Kumekuwa na kitendo vya utovu wa nidhamu katika kata hii kwani watu wamekuwa wakilima na kuuza bangi hadharani hivyo kuanzia sana ni marufuku kuendesha biashara yoyote ya madawa ya kulevya hapa Mlali"alisema Sanare.

**Kuanzia sasa kutakuwa na ulinzi mkali katika maeneo yote ya kata hii kwani lengo ni kutaka kukomesha kilimo na matumizi ya bangi hapa Mlali na kwamba mtu yeyote atakayekamatwa familia yake isije ikalaumu serikali.**

Mkuu huyo wa mkoa alisema kilimo cha bangi na matumizi yake hakikubaliki hapa nchini na mtu kuendesha kilimo za zao hilo ikiwa ni pamoja na matumizi ya biashara ya zao hilo ni uvunjifu wa sheria hivyo wananchi wanatakiwa kuliepuka.

Alisema yapo mazao mengi ya kibiashara yanayolimwa maeneo mbalimbali hapa nchini hususani kwa mkoa wa Morogoro ambapo aliwataka wananchi wa kata hiyo kuwekeza kwenye mazao hayo na siyo kujihusisha na kilimo cha bangi.

"Kuanzia sasa kutakuwa na ulinzi mkali katika maeneo yote ya kata hii kwani lengo ni kutaka kukomesha kilimo na matumizi ya bangi hapa Mlali na kwamba mtu yeyote atakayekamatwa famila yake isije ikalaumu serikali," alisema Sanare.

Alisema kuwa uchunguzi umebaini kuwa wilaya ya Mvomero inaongoza kwa vitendo viovu ikiwamo suala la migogoro mbalimbli na kwamba sababu kubwa ni utumiaji wa bangi ambapo amewataka watendaji wa vijiji na kata kuwa makini.

Ole Sanare alesema watendaji wa vijiji pamoja na kata ndiyo wanatakiwa kuwa mstari wa mbele hukakikisha kilimo na matumizi ya bangi yanakwisha kabisa eneo hilo ambapo amewata kuacha tabia ya kuufumbia macho uovu huo wote.

Katika hatua nyingine Mkuu huyo wa mkoa aliagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuchunguza wale wote wanaohusika na ubadhirifu wa fedha zinazotolewa ajili ya ya maendeleo katika kata hiyo.

Kwa upande wao wananchi wa kata hiyo walimuomba mkuu hiyo wa mkoa kuwasaidia kudhibiti Tembo ambao wakekuwa wakivamia kakazi yao na kutishia usalama wa maisha yao kwa ujumla hususani majira ya usiku kila wakati.

Kulwa Adam ni mkazi wa kata hiyo alisema kwa hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la tembo kutoka Hifadhi ya Mikumi na kuvamia makazi ya wananchi na kusababisha uharibifu ambapo aliiomba serikali iwasaidie kuwadhibiti tembo hao.



Wafanyabiashara wakiwa wamepanga bidhaa zao chini katika Soko la Temeke, jijini Dar es Salaam juzi kitendo ambacho ni hatari kwa afya ya walaji. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Mradi kutetea haki za wazee watambulishwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

KATIKA kupambana na vitendo vya kikatili na mauaji ya vikongwe mkoani Shinyanga, shirika lisilo la kiserikali la kutetea wazee (TAWLAE) limetambulisha mradi wa kulinda na kutetea haki za wazee hasa wanawake, kutokana na vitendo vya kikatili na manyanyaso.

Mradi huo utatekelezwa katika kata tisa na vijiji 36 vilivyopo katika Halmashauri ya Mji wa Kahama na lengo la mradi huo ni kutokomeza vitendo vya kikatili kwa wazee hasa wanawake ambavyo vimekuwa vikijitokeza mara kwa mara.

Akitambulisha mradi huo jana kwa Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, Mratibu wa TAWLAE mkoani Shinyanga, Winnie Hinaya, alisema mradi huo utasaidia kupunguza vifo vya wazee kwenye kata zenye changamoto za wazee kwa asilimia 98.

Alisema mradi utatekelezwa kwenye kata tisa, vijiji 36, Halmashauri ya Mji wa Kahama na wanatarajia kuwafikia zaidi ya wazee 15.617 masikini, wajane wazee, walemavu na kumtaka Ofisa Ustawi wa Jamii na viongozi wa baraza la wazee Halmashauri kushirikiana kutatua changamoto za wazee.

Nae Meneja mradi wa Helpage International, Joseph Mbasha, alisema mauaji ya vikongwe yanayotokana na imani za kishirikina yamepungua kwa kiasi kikubwa na mwaka 2023 shirika litahakikisha hakuna matukio ya mauaji yatakayoripotiwa tena.

Hata hivyo, alisema mwaka 2000/2015 matukio ya mauaji ya vitendo vya kikatilia kwa wazee na wenye ulemavu wa ngozi nchini nzima yalikuwa 700 hadi 500, huku mwaka 2016/17 vilikuwa 350 hadi 100 na mwaka 2018/19 vilikuwa 56 hadi 13.

Mwenyekiti wa baraza la wazee la Halmashauri ya Mji wa Kahama, Wilfred Birago, alisema mwaka wa fedha 2018/2019 Halmashauri ilitenga Sh. milioni 11.7 na kuwakatia bima za afya ya CHF zaidi ya wazee 3,380 na kurahisisha huduma za afya kwa wazee.

# AJISO yazindua kamati za kutokomeza ukatili

**Na Mwandishi Wetu**

KUTOKANA na kuongezeka kwa vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto wilayani Mwanga, Shirika la Action for Justice in Society (AJISO) kwa kushirikiana na uongozi wa wilaya hiyo, wamezindua na kuzijengea uwezo kamati mbili zitakazokabiliana na tatizo hilo.

Kamati hizo zinaundwa na wajumbe kutoka Kata za Lembeni na Kirongwe wilayani Mwanga, wajumbe 50 ambao ni mchanganyiko wa wadau mbalimbali wakiwamo viongozi wa kata, viongozi wa dini, walimu na wanafunzi wamepata mafunzo ya siku mbili, ili kutekeleza vizuri Mpango wa Taifa wa Kupinga Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) kupitia mradi wa TUWALINDE.

Wakati wa uzinduzi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga, Zefrin Lubuva, alisema suala la ukatili dhidi ya watoto na wanawake ni tatizo kubwa katika wilaya yake, hivyo walilazimika kuomba msaada kutoka AJISO ili kutekeleza mafunzo hayo na kuhakikisha kamati zinafanya kazi kwa ufanisi.

Alisema wilaya hiyo ina kata 20, lakini hadi sasa ni kamati tatu tu zilizojengewa uwezo, akifafanua: "Tunatamani kamati zote 20 zifikiwe ili kwa pamoja tuweze kutokomeza suala hili la ukatili dhidi ya watoto na wanawake."

Mkurugenzi huyo alizipongeza kamati hizo kwa kukubali kufanya kazi hiyo ya kujitolea zaidi kwa manufaa ya watoto na wanawake katika jamii.

"Uongozi wa wilaya utaendelea kushirikiana na AJISO na mashirika mengine yenye lengo la kutokomeza ukatili dhidi ya watoto na wanawake katika Wilaya ya Mwanga," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa AJISO, Virginia Silayo, alisema wamepokea ufadhili wa Sh. milioni 30 kutoka Shirika la Foundation for Civil Society ambazo zitasaidia katika kutekeleza mradi huo kwa muda wa miezi sita kuanzia Juni hadi Desemba mwaka huu.

Alisema hapo awali waliijengea uwezo kamati moja ya Kata ya Mji Mdogo wilayani huko na imekuwa ikifanya vizuri na kupata sifa nyingi kutoka mkoani kwa namna ilivyopambana na ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, baada ya hapo waliamua kuja na mkakati wa ulinzi wa mtoto, ili utumike katika shule hiyo na baadaye walikaa na wadau mbalimbali na kuboresha ili utumike katika shule zote za Wilaya ya Mwanga kutokana na mafanikio yake.

# Hamasa 2020 zilivyoibua wanawake wengi kutiania

Ukurasa 13





siasa
JUMATANO JULAI 22, 2020
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU




Ukurasa 12

## Mbunge alivyobadilishia gia angani, alia kutusiwa

# Wanaodai Ikulu imewatuma wangejiuliza walifeli wapi?

**Na Magabilo Masambu, ARUSHA**

ITAKAPOWADIA Oktoba mwaka huu, ndiyo wakati wa uchaguzi mkuu wa madiwani, wabunge na urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na jana matokeo ya wagombea wa CCM yameanza kutangazwa baada ya mchakato wa awali wa kura za maoni kutangaza nia na kuchukua fomu za kugombea, kuna jambo limejitokeza ambalo huenda litasukuma umma kulitafakari na watia nia wa ngazi za ubunge na udiwani kujipima wanapoelekea kwa wananchi na wajumbe wa kamati mbalimbali za siasa ambazo zina mamlaka ya kupitisha majina yao.

Wengi katika kujinadi wanajihalalishia kutafuta uongozi kwa kutumia jina la Rais John Magufuli, ambaye ni rasmi amewakana.

Wengine wanatoa msururu wa maelezo mfano:"Nimeamua kugombea kwasababu Rais amejenga barabara, ameleta maji, amenunua ndege, ametoa elimu bure, amejenga reli ya kisasa, ametatua tatizo la mgawo wa umeme, amejenga na kuhamishia makao makuu ya nchi Dodoma."

Aidha, wanataja mambo mengi, mengine ni jambo jema lakini wanaomsikiliza huenda wanawaza na kuona kuwa kwa sababu yote hayo yamefanywa kwa usimamizi wake yeye kama kiongozi wa ngazi ya juu wa serikali anayehusika na kusimamia na kuleta maendeleo. Lipo swali kwa mgombea, kama yote hayo yamefanyika anaomba nafasi ya ubunge ili akafanye yapi?

Katika serikali ambazo zinaongozwa kidemokrasia kama Tanzania uongozi unakuwa shirikishi na serikali ni ya wananchi, katiba inaeleza.

### SEMA YAKO SI YA JPM

Ibara ya 8(1) inasema Tanzania ni nchi inayofuata misingi ya demokrasia na haki za kijamii na kwa hiyo, wananchi ndiyo msingi wa mamlaka yote na serikali inapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi.



Rais John Magufuli akikagua ujenzi wa reli ya kisasa-SGR . Baadhi ya wagombea hutumia kazi alizofanya Rais kama mtaji wa kutaka uongozi. **PICHA: MTANDAO.**

Inasema lengo kuu la serikali litakuwa ni ustawi wa wananchi na itawajibika kwa wananchi tena watashiriki katika shughuli za serikali yao kwa mujibu wa masharti ya katiba. Ni wazi si kosa kwa mujibu wa sheria kusema Rais kafanya mambo kadhaa inajulikana anayeongoza ni nani lakini pia unakuwa umewataja pia viongozi walioko ngazi zote kutoka vijijini hawa nao si wa kupuuza.

Mara kadhaa Rais Magufuli amesikika akisema Watanzania watembee kifua mbele kwasababu wameweza kufanya mambo yao wenyewe bila mikopo wala kuomba omba maana yake anatambua kuwa yeye pekee hawezi yuko na wananchi. Kwahiyo, mgombea anapotaka kukubalika kwa wapiga kura kwa kutumia jina la Rais kwa namna yoyote ile hatakuwa tofauti na tapeli ndiyo maana Rais akiwaapisha viongozi mbalimbali aliowateua hivi karibu anasisitiza na kurudia kusema kwamba hajatuma mgombea.

Anawaonya wanaowatishia wajumbe kuwa wametumwa na Rais kugombea, ndiyo maana anaonya kuwa hajamtuma yeyote akagombee mahali popote na akaongeza kuwa si Makamu, Waziri Mkuu, Mkuu wa Majeshi au yeyote aliyemtuma yeyote kugombea popote kwa hiyo akajiondoa kwenye madai ya kumsingizia.

### WAGOMBEA JITEGEMEENI

Wagombea simameni kama ninyi waambieni wananchi mnataka kuwafanyia nini si kile Rais Magufuli, alichofanya.

Semeni mnataka Rais atakapoanza kampeni akose cha kusema? Mnageuka kuwa mameneja wa kampeni ya mgombea wa urais?

Kazi hiyo Watanzania wanafikiri ataifanya atakayeteuliwa kuwa meneja kapeni lakini si wagombea ambao hujitutumua kwa kuelezea mafanikio ya Rais.

### MMEJIPIMA, MNATOSHA

Viongozi wajipime na kujitazama kwani unapoamua kuchukuwa fomu ya uongozi umeshajihakikishia kwamba unaweza kuuzika wewe mwenyewe binafsi bila kuuzwa ndiyo maana masuala ya uongozi si ya kukurupuka.

Wanaotumia jina la Rais walitakiwa wawe na maandalizi ya kutosha yasiweya elimu na fedha tu, hata kama kuna wanaokuambia kuwa unafaa wakubalie lakini waambie nadhani nahitaji muda zaidi wa kujiandaa vema kwasababu uongozi lazima kwanza watu watambue dhamira yako kabla ya kuwafanya wakuamini.

Sababu zinazofanya watu wamkubali mgombea 'A' haziwezi kumfanya ' B' akubalike pia, kwenye siasa jifunze kusimama peke yako bila ushawishi wa mtu mwingine wa pembeni. Ndiyo maana Rais amewakataa kwani mgombea huwezi kukubalika kwasababu kuna mambo yalifanywa na mwingine wewe sema yako yatakayokufanya upigiwe kura.

Kuna baadhi ya wagombea wanabebwa na jina la chama, na wapo wanaokibeba chama ili uwe mgombea bora pengine ni vyema uhakikishe kwanza ndiye unayeweza kukibeba chama yaani watu wasichague chama badala yake wakuchaguwe wewe binafsi kwasababu chama hakitafanya kusudi lako kwa wananchi.

Kujiamini huko kumewapofusha viongozi wengi ambao walishinda kwa kishindo kwenye uchaguzi uliopita wakadhani walishinda kwasababu wao wanakubalika kumbe walitakiwa baada ya ushindi wajifanyie tathimini kujipima ikiwa wao ndiyo walishinda au chama?

Kama wangejifanyia tathimini ingekuwa chachu ya kung'amua mapema ili kujipanga vizuri lakini kwa wengine sivyo. Kuna wanaosema nilishinda kwa kura nyingi sana.

### KUJIPA SIFA

Wagombea wanaotambia ushindi wajihoji walishinda wao au chama chako? Wajitambue kuwa wanagombea nafasi ya udiwani na ubunge si ya urais kudai kwamba nimeamua kugombea kwasababu katika jimbo hili Rais amefanya mengi hata siwezi kueleza ni kuwaambia wananchi wasikuchague bali wampe Rais nafasi.

Ni wazi wana CCM maelfu wamejitokeza kutumia haki yao ya kuomba ridhaa na ni jambo jema kwamba sasa siasa si ya wazee kama ilivyozoeleka vijana wameamka kuomba uongozi wa ubunge au udiwani kuleta mabadiliko na si kwa nia ya kutega ili kupata uteuzi mbalimbali kama yanavyozungumzwa huko mitaani.

Kwa wapigakura ni muhimu wakajitokeza kwa wingi kuwasikiliza wagombea ikibidi kuwaeleza kuwa hakuna aliyetumwa kugombea wawaulize maswali, wachuje hoja na kubwa kupima uwezo na uwelewa wao na isiwe wanagombea kisa Rais amefanya mambo makubwa kwa miaka mitano. Tena isiwe ni kutamani tonge na kulisaka zaidi.

***Maoni: 0689157789/0758379296, magabilomjalifu@gmail.com***

# Mbunge alivyobadilishia gia angani, alia kutusiwa

## •Ajiengua dakika za majeruhi



Lameck Airo akihutubia kwenye moja ya mikutano yake alipokuwa mbunge wa jimbo la Rorya. **PICHA: MTANDAO**

**Na Sabato Kasika**

MBUNGE wa Rorya mkoani Mara anayemaliza muda wake, Lameck Airo, ameshindwa 'kutesti mitambo'. Akiwa miongoni mwa zaidi ya makada 40 wa CCM, waliochukua fomu kutetea nafasi iliyokuwa akiishikilia ameingia mitini bila kurejesha fomu.

Kutokana na kukwama kurudisha fomu, kimya kimya amewatangazia wapigakura wake kuwa amejitoa kuwania ubunge wa jimbo hilo jambo alilililofanya katika dakika za majeruhi.

Katika maelezo yake, mwanasiasa huyo anasema, hakuwa na mpango wa kuwania ubunge, bali alichokuwa akifanya ni 'kutesti mitambo' tu, na kuwaachia wanaotaka kiti chake waendelee.

Airo alichukua fomu za kuomba kupitishwa kuwani jimbo hilo, Julai 17 ambayo ilikuwa ni siku ya mwisho ya uchukuaji na urejeshwaji wa fomu hizo, lakini akatangaza kujiondoa kwenye kinyang'anyiro hicho.

> Nilikuwa 'natesti' maana nilishawaahidi wananchi kwenye mikutano yangu kuwa sitogombea napumzika lakini cha ajabu baadhi ya wana Rorya wakiwamo wasomi wakawa wananitukana kwenye mitandao ya kijamii mara...

"Nilikuwa 'natesti' maana nilishawaahidi wananchi kwenye mikutano yangu kuwa sitogombea napumzika lakini cha ajabu baadhi ya wana Rorya wakiwamo wasomi wakawa wananitukana kwenye mitandao ya kijamii mara mimi ni darasa la saba naongozaje na wasomi wapo? Nimevumilia mengi sana na hao waliokuwa wananitukana baadhi yao ni wasaliti wa chama na leo wametia nia kugombea," anakaririwa na vyombo vya habari akisema.

Anafafanua kuwa alipoona wanamuandama akachukua fomu ili ajipime na hao wasomi, na kwamba waliposikia amechukua fomu wakaanza tena kupata presha kulalamika, ndipo akatafakari zaidi na kubaini kuwa hana haja ya kusumbuana kwa vile Rorya ni yao sote.

Anasema ameamua kujiondoa kwa roho moja ili na wasomi waongoze na kwamba atakayeshinda atamuunga mkono kwa maslahi ya Rorya na kuwataka wasiwe na shaka kuhusu ushirikiano wake.

"Nimezaliwa Rorya, hivyo naahidi kutoa ushirikiano, ila namtaka atakayechaguliwa mbunge asiishie kukaa mjini afike jimboni ashiriki maendeleo kwa juhudi zote hata kama kipato chake ni kidogo lakini msaada wake utasaidia kulingana na uwezo wake," anasema mbunge huyo anayeng'atuka dakika za mwisho.

### ALIVYOSITASITA

Aprili mwaka jana, Airo alikaririwa na Nipashe akisema kuwa baada ya mwaka huu asingerudia kuwania ubunge, huku akiwa na sababu mbalimbali, mojawapo ikiwa ni kuheshimu utaratibu wa kuachiana vijiti.

Nyingine anaitaja kuwa ni kupata muda wa kusimamia biashara zake, kuacha uongozi akiwa bado na nguvu na akipendwa na wapigakura kuliko kusubiri kuchokwa na kama ambavyo imekuwa ikitokea kwa baadhi ya wanasiasa.

Anasema kwamba, yeye siyo kama walivyo wanasiasa wengine ambao hufanya uamuzi kwa ajili ya kuwajaribu wapigakura na kisha baadaye wanachukua fomu kuwania ubunge, hawezi kufanya hivyo.

Lakini pamoja na ahadi hiyo, Airo amejikuta akiiweka pembeni na kubadili gia angani ya kuchukua fomu ya kuwania ubunge, kisha akaamua kujiondoa akidai kwamba alikuwa anatesti mitambo.

Kimsingi ana haki ya kuchagua au kuchaguliwa, lakini mkanganyiko unakuja kwenye uamuzi wake wa awali ambao amewahi kuutoa, halafu baadaye anauweka pembeni kimya kimya na kuchukua fomu.

Kama ambavyo amewahi kutangaza kwenye vyombo vya habari kwamba, safari hii hagombei tena ubunge, hata hatua ya kurudi kwenye kinyang'anyiro angaitangaza pia hadharani, kwa sababu siyo kosa.

Yawezekana wapigakura walikuwa bado wanamhitaji wakaamua kumshauri abadili msimamo wa awali.

Mbali na Airo, wapo baadhi ya wabunge ambao tangu mwaka jana, walitangaza kustaafu na kwenda kuwaaga wapigakura wao na pia wabunge wenzao bungeni.

Miongoni mwao ni aliyekuwa mbunge wa Muleba Kusini mkoani Kagera, Profesa Anna Tibaijuka, ambaye hakubadili uamuzi wake huo wa kustaafu kama ambavyo baadhi ya makada wamefanya.

Yeye hakuwa miongoni mwa makada zaidi 10,000 wa CCM nchi nzima, ambao wamechukua fomu za kuwania ubunge katika majimbo mbalimbali ya uchaguzi wakiwamo wa viti maalum pia.

Hivyo suala la kusimamia uamuzi ni la msingi ili kuondoa mkanganyiko kama huo ambao imetokea Rorya baada ya mbunge mstaafu kuchukua fomu za kuwania ubunge huku akiwa ameutangazia umma kuwa hagombei.

Wakati anatangaza kustaafu, anasema, uamuzi wake ni unazingatia kauli ya Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ya kuhimiza kung'atuka ili kupisha mawazo mapya hasa ya vijana.

Amesimamia uamuzi huo ambao baadhi ya watu walikuwa wakiutilia shaka kwamba wanasiasa huwa hawaeleweki, wanaweza kwenda kinyume na kile wanachoahidi, hivyo ni vyema kusubiri hadi mwisho.

Waliokuwa wakidhani kwamba anaweza kubadilika baadaye, watakuwa wameshuhudia jinsi alivyosimamia kile alichoamua, kwani hadi uchukuaji na urejeshwaji wa fomu za kuwania ubunge ndani ya CCM jina lake halimo.

# Hamasa 2020 zilivyoibua wanawake wengi kutiania




Mwantumu Mussa Sultan mmoja wa watiania wa urais wa Zanzibar 2020. **PICHA :MTANDAO.**

**Na Ani Jozeni**

HARAKATI za kuwapata wagombea ubunge na udiwani zinaelekea ukingoni baada ya wanachama kukamilisha mchakato wa kujaza na kurudisha fomu na kinachosubiriwa sasa ni kipenga cha kampeni za uchaguzi mkuu, unaotarajiwa kufanyika mwishoni mwa Oktoba.

Yaliyojitokeza hadi sasa ni wingi wa watiania katika maeneo kadhaa, ambao kwa upande wa CCM ni wanaotaka nafasi za ubunge, wakati Chadema imeonyesha kuwa na wengi au kadhaa kutaka nafasi ya kugombea urais.

Mathalani katika kuomba kuteuliwa kwenye uchaguzi wa urais wa Zanzibar walikuwa watiania 32 kati yao wanawake walikuwa watano.

Kitaifa CCM ilikuwa na watiania 10,367. Dar es Salaam pekee walijitokeza ni 1,426 kati yao watiania kwenye udiwani ni 2,801. Namba hiyo ni kubwa na haijawahi kufikiwa.

Vyama vingine vya upinzani vilikuwa vinasuasua maeneo yote mawili, mbali na ACT-Wazalendo ambayo tayari ina wagombea urais wa Muungano na Zanzibar, hapakuwa na msukumano wa kuchukua fomu kwa ngazi hiyo.

Kingine kilichojitokeza ni wanawake wengi kuchukua fomu, hasa Chadema hasa kwa ajili ya kugombea ubunge, ambao inaelekea ni mkakati maalum ndani ya chama hicho, kwani siyo mara ya kwanza suala hilo limezungumziwa au kuashiriwa.

Mwaka 2018 wakati wa sikukuu za Muungano na Siku ya Wafanyakazi, ilipozuiliwa kuandaa maandamano yote kichama, wanawake wa Chadema wilayani Chato walijipanga na kukusanyika kichama, kuandamana hadi ulipokuwepo mkutano wa hadhara wa wana-CCM.

Taarifa za mitandaoni wakati huo hazikuonyesha kwa kuna nini kilitokea baada ya hapo, kama uwepo wa wageni hao kutoka Chadema ulitambuliwa na kukaribishwa kama sehemu ya sherehe hiyo. Isingekuwa rahisi kufanya hivyo ila ingeendana na taarifa rasmi kuwa huo ni mkusanyiko wa kitaifa na siyo wa chama, licha ya washiriki kuvaa sare takriban wote na waliokuja wanadaiwa hawakuwa na sare nyingi, wakionekana kama kundi la wananchi waliokuja kushiriki mkutano, wakiimba.

> Mwaka 2018 wakati wa sikukuu za Muungano na Siku ya Wafanyakazi, ilipozuiliwa kuandaa maandamano yote kichama, wanawake wa Chadema wilayani Chato walijipanga na kukusanyika kichama, kuandamana hadi ulipokuwepo mkutano wa hadhara wa wana-CCM.

Hivi karibu chama hicho kilitoa msimamo kuwa jumuiya ya wanawake wa chama hicho ni nguzo muhimu ya kampeni au uhamasishaji katika na kwamba katika uchaguzi mkuu hicho ndicho kitakachotokea.

Ziko sababu kadhaa za kuunda mkakati kama huo, kwani kwa upande mmoja kuna harakati nyingi za kitaifa zinazohusisha hasa makundi huria kama vyama vya kijamii au visivyo vya kiserikali, licha ya kuwa wapo wengine wanaona ni matawi ya makundi ya nchi za nje yenye ajenda za kimataifa. Ndiyo vinara wa mkakati wa usawa wa kijinsia unaobeba ajenda ya 50-50 katika uwakilishi, kama lengo linalohitaji kufanyiwa mikakati ili kulitimiza.

Ila kufikia azma hiyo unahitajika mkakati unaokidhi kwa vitendo lengo la kuwafanya wanawake kuwa mstari wa mbele na washiriki wakuu wa shughuli za uchaguzi mkuu wa sasa na mmoja hadi mwingine kwa kuhimiza ushiriki wa wanawake na pia kuchaguliwa katika nafasi walizoomba.

Ndiyo hapo unakuja mtihani kwa wanaharakati kuhusu mkakati wa jumla wa uwiano uwakilishi na madaraka kwa jumla kwa upande mmoja na dhana za kitaaluma (au kisayansi) zinazoweka msingi wa mkakati huo.

Ni suala la kuendelea na utafiti wa kiuhalisia kuhusu uwezekano wa mkakati huo, kwa njia gani, kwa kipindi gani utatelekezwa.

Kwanza kuna hatua ya kuchukua fomu na kupata wadhamini kwa nafasi wanayotaka kugombea, kama kutakuwa na vikwazo kwa baadhi yao ukilinganisha na wanaume waliotia nia kama hiyo, hali ambayo kwa jumla haitazamiwi kuwepo.

Halafu kuna kupigiwa kura na wajumbe wa mikutano hasa ya ngazi ya jimbo, wilaya, mkoa na mkutano mkuu ambao ni ngazi ya kitaifa wanaotaka kugombea nafasi ya urais.

Kwa upande wa Chadema amejitokeza mwanamke mmoja kwa nafasi hiyo naye ni Dr. Maryrose Majige.

Suala la kuongeza uwakilishi bungeni kwa upande kwa wanawake, nje ya viti maalum vinavyotolewa kulingana na idadi ya wabunge waliopo, litaendelea kuwasumbua wanaharakati.

Kimsingi suala la uwepo wa wanawake katika vyombo vya uwakilishi linatatuliwa na viti maalum, kwani mengine yanategemea kipaji cha mhusika na kukubalika kwa wananchi.

Kukosa kura kutokana na jinsia peke yake si mwelekeo wa wapigakura walio wengi, ila ziko nafasi, kwa mfano ngazi ya urais, bado itakuwa ngumu.

Mambo yamebadilika kwa upande mwingine unaweza kusema kuwa hata Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan, anaelewa kuwa CCM haina tabu kukubali mwanamke kuwa mgombea.

Kwa sasa ina maana kuwa harakati ya jumla za 50-50 inawezekana hazijatilia maanani umuhimu wa utamaduni ambao unaendana na nafasi ya wanawake kijamii, suala ambalo hata katika fani nyingine za kijamii linaleta utata.

Pale ambapo kinachotakiwa ni taaluma peke yake, hakuna tatizo wanawake kupewa nafasi za juu, na hata katika ngazi za utawala, kufikia hata Baraza la Mawaziri au umakamu wa rais. Ila pale ambapo watu wenyewe wanatafuta mwakilishi, mpambanaji, ushindani unawaelemea wanawake, hivyo kupata mafanikio ya mkakati wa 50-50 haitakuwa rahisi, hivyo wanaharakati wasivibeze viti maalum.

# DAG HAMMARSKJÖLD

- Katibu Mkuu UN aliyeuawa akiisotea Congo
- Alifia Zambia, miaka 59 uchunguzi wa kifo



Dag Hammarskjöld (chini), enzi za uhai wake. Juu ni mabaki ya ndege yake iliyoangukia Ndola Zambia miaka 59 iliyopita. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Mwandishi Wetu**

SEPTEMBA mwaka huu inatimia miaka 59 ya kifo cha Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Dag Hammarskjöld, aliyepoteza maisha yake akiisotea amani ya Congo.

Septemba mwaka 1961 ndege yake ilianguka katika ardhi ya Zambia, wakati wa ziara ya kidiplomasia kujaribu kuleta mapatano na kusitisha vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini Congo.

Awali ilielezwa kuwa makosa ya rubani ni sababu ya kuanguka kwa ndege hiyo, hata hivyo ushahidi mpya umeibuka ambao huenda ukaongeza shaka kuwa ajali hiyo ilipangwa.

Ili kuchunguza ajali hiyo, Umoja wa Mataifa uliazimia kuilazimisha nchi hiyo kusalimisha nyaraka na sauti za mawasiliano ya radio kwa uchunguzi maalum ambao huenda ukafichua ukweli kuhusu kile kilifanyika na kumuua Hammarskjold na wasaidizi wake walikuwa wakielekea Ndola Zambia, kukutana na Moise Tshombe ambaye alikuwa ametangaza uhuru wa eneo lenye utajiri wa madini la Katanga.

**BADO NI KITENDAWILI**

Mwaka 2018, kwa mara nyingine UN kupitia Katibu Mkuu Antonio Guterres, ilianzisha uchunguzi mpya wa kifo chake na kumteua Jaji Mkuu mstaafu wa Tanzania, Mohammed Chande Othman kuongoza jopo la uchunguzi wa kifo cha Dag Hammarskjöld.

> Hammarskjöld aliyekuwa Katibu Mkuu wa pili wa Umoja wa Mataifa, alifariki dunia Septemba 18, kwenye ajali ya ndege wakati akiwa safarini kusaka amani kwenye iliyokuwa Zaire ambayo sasa ni Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo- DRC.



Hammarskjöld aliyekuwa Katibu Mkuu wa pili wa Umoja wa Mataifa, alifariki dunia Septemba 18, kwenye ajali ya ndege wakati akiwa safarini kusaka amani kwenye iliyokuwa Zaire ambayo sasa ni Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo- DRC.

Uteuzi wa Jaji Othman ulifanywa kwa mujibu wa Azimio namba 72/252, la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa ambapo uteuzi wake ulijumuisha pia jopo la wajumbe wengine waliokuwapo hapo awali. Wataalamu wengine wanatoka Australia na Denmark.

**DAG ALISHAMBULIWA?**

Hadi sasa ripoti ya uchunguzi wake ilihitimisha kuwa bado kuna maswali na masuala mengi yaliyosalia kuhusu uwezekano kuwa pengine shambulio kutoka nje ya ndege hiyo linaweza kuwa sababu ya kuanguka.

Mwaka 2015 UN ilitaka taarifa kuhusu ajali ya ndege ya Hammarskjold, ikiidhinisha kwa kauli moja azimio linalozitaka nchi zote, kutoa taarifa zote zinazohusu ajali ya ndege ya mwaka 1961, iliyomuuawa Dag Hammarskjold.

Julai 2015 wakati huo Katibu Mkuu wa UN akiwa Ban Ki-Moon aliliambia Baraza Kuu la UN kuwa uchunguzi umegundua taarifa mpya inayoonyesha kuwa ndege hiyo ilishambuliwa ikiwa angani au uwezekano wa kuingiliwa kwa aina yoyote nyingine, hivyo wanataka uchunguzi zaidi ufanyike.

**HISTORIA**

Dag Hammarskjold, aliyekuwa raia wa Sweden, alichaguliwa Katibu Mkuu wa pili wa Umoja wa Mataifa mwaka 1953, aliuawa pamoja na watu wengine 15, wakati akiwa njiani kuelekea Kongo ili kuwapatanisha viongozi wa Congo na muasi Congo.Ndege yake ilianguka na watu wote walioteza maisha

Jopo la wajumbe watatu lililoteuliwa na Ban, limetoa wito wa kuwepo taarifa maalum kutoka Ubelgiji, Ufaransa, Ujerumani, Afrika Kusini, Marekani na Uingereza, katika kipindi cha uchunguzi kuhusu ajali hiyo iliyotokea Septemba mwaka 1961. Jopo hilo lilisema maswali yote hayakujibiwa ipasavyo.

Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa lenye wanachama 193 lilipitisha azimio linalozitaka nchi zote wanachama, hasa zile zilizoorodheshwa kwenye ripoti ya kurasa 99, kutoa taarifa sahihi walizonazo zinazohusiana na kifo cha Hammarskjold na kuziwasilisha kwa Katibu Mkuu na kumuomba Ban kuteua jopo huru la wataalamu watakaochunguza kifo hicho na kutoa taarifa mpya.

**MAZINGIRA YA KUANGUKA**

Ripoti ya jopo hilo la awali imeeleza kuwa kutokana na taarifa zilizotolewa na watu tisa walioshuhudia, walisaidia kubaini kwamba kulikuwa na ndege nyingine angani.

Yaliyotokea yanaelezwa kuwa wakati ndege ya Hammarskjold chapa DC-6 ilipokuwa inakaribia kutua katika uwanja wa ndege au ndege ya katibu mkuu huyo wa zamani, ilishika moto kabla haijafika ardhini au ililipuliwa na ndege nyingine wakati ikikaribia kutua Ndola.

**MAREKANI KUHUSIKA**

Taarifa za vyombo vya habari ikiwamo UN News, zilidai kulikuwa na taarifa mpya za ziada kwamba Wamarekani wawili, Charles Southall, Kamanda wa zamani wa Jeshi la Maji la Marekani na Paul Abram, ofisa wa zamani wa idara ya kikosi cha usalama cha anga, huenda walisikiliza au walitafsiri matangazo ya redio usiku wa Septemba 17-18 mwaka 1961, ambayo wanaamini yalikuwa yakiripoti kuhusu shambulizi la ndege ya Hammarskjold ambayo ilichangia kuanguka kwake.

Jopo hilo lilisema Uingereza imekataa kutoa mafaili yanayoonyesha shughuli za shirika la ujasusi la nchi hiyo katika eneo la Katanga. Jopo hilo lilipata nyaraka za ushahidi kutoka taasisi ya utafiti wa bahari ya Afrika Kusini, zinazoonyesha kufanyika kwa "operesheni Celeste", kwa ajili ya kumuondoa, Hammarskjold, kwa ushirikiano na mkurugenzi wa shirika la ujasusi la Marekani-(CIA), Allen Dulles.

Kwa mujibu wa jopo hilo, nyaraka hizo zilionyesha kuwa kiongozi huyo wa zamani wa Umoja wa Mataifa, angekuwa Leopoldville Septemba 12, mwaka 1961.

***MITANDAO.***



HABARI DODOMA

# Askofu akemea wagombea kuendekeza ushirikina

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

ASKOFU wa Kanisa la Pentecostal Holiness Association Mission Tanzania (PHAMT) Kanda ya Kati, Julius Bundala, amewataka wagombe katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu, kujiepusha na vitendo vya kishirikiana.

Askofu Bundala alitoa rai hiyo jana alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu uchaguzi huo uliopangwa kufanyika Oktoba 28 mwaka huu.

Alisema kama wagombea wote watamtanguliza Mungu katika uchaguzi huo, vitendo vya mauaji ya watu wenye ualbino na vikongwe havitakuwapo nchini.

"Wagombea wote wanatakiwa kuwa na hofu ya Mungu, pamoja na kumtanguliza Mungu mbele kwanza na siyo kujihusisha na vitendo vya kishirikina ili kuchaguliwa," alisema.

Alisema kuwa kama wagombea hao watajihusisha na nguvu za giza badala ya kumtegemea Mungu, taifa litapata viongozi ambao siyo waadilifu watakaorudisha nyuma jitihada zote ambazo zimefikiwa katika miaka mitano iliyopita.

Alisema wagombea wote pia wanatakiwa kuacha kutumia lugha za matumizi wakati kampeni zitakaoanza, ili kuwa na uchaguzi huru na wa haki.

"Kila mgombea anapaswa kutoa sera zake pamoja na chama chake, na siyo kujihusisha na kampeni za matusi kwa wagombea wenzake, hali hii inaweza kusababisha ufunjifu wa amani iliyo katika taifa letu," alisema.

Askofu Bundala pia aliwataka viongozi wa dini nchini kuendelea kuliombea taifa katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi.

"Viongozi wa dini pia tunao wajibu kuhimiza waumini wetu, kushiriki kikamilifu katika uchaguzi mkuu mwaka huu, ili watimize wajibu wao wa kikatiba wa kumchagua kiongozi atakayewaongoza katika miaka mingine mitano," alisema.

"Tunamwomba Mungu alete viongozi ambao wataweza kuendeleza kazi hii nzuri ili kuendeleza maendeleo haya pamoja na kuongeza kasi zaidi ya kuyafikia maendeleo ya juu," alisema.

# TARURA yafanya utafiti lami baridi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAKALA wa Barabara ya Vijijini na Mijini (TARURA), kwa kushirikiana na Kampuni ya Starpeco Limited ya jijini Dar es Salaam, wanafanya utafiti wa matumizi ya teknolojia ya lami baridi Jiji la Dodoma, ili kuangalia kama itafaa kutumika kwenye ujenzi wa barabara zinazosimamiwa na wakala huo.

Meneja wa TARURA Mkoa wa Dodoma, Mohammed Makwata, aliyasema hayo jana alipofungua semina ya wanafunzi wa Vyuo vya Ufundi Standi (VETA) nchini ambao walikuwa wakipewa uelewa kuhusu teknolojia hiyo.

Alisema utafiti huo unafanywa kwenye barabara yenye urefu wa kilometa mbili na itakapobainika kuwa lami hiyo ina ubora, itaanza kutumika kwenye barabara za TARURA.

**teknolojia ya lami baridi imetumika pia katika ujenzi wa Barabara ya Bagamoyo, TAZARA Flyover, Ubungo Flyover ambapo kwa sasa wanakarabati barabara darasa katika Jiji la Dodoma.**

"Kama teknolojia hii itaonekana kufanya vizuri, tutaruhusu kutumika maeneo mbalimbali nchini, kwani tuna mtandao mkubwa wa barabara na TARURA ina barabara nyingi zinazohitaji kujengwa na kutumika nyakati zote kwa maendeleo ya uchumi wa nchi," alisema.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Starpeco Limited, Gratian Nshekanabo, alisema kampuni yake imeweka viraka katika barabara za Changanyikeni na Uvumbuzi zilizoko Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Alisema teknolojia ya lami baridi imetumika pia katika ujenzi wa Barabara ya Bagamoyo, TAZARA Flyover, Ubungo Flyover ambapo kwa sasa wanakarabati barabara darasa katika Jiji la Dodoma.

Alizitaja barabara zitakazowekwa lami hiyo kuwa ni zile zenye majina ya viongozi wakuu wa nchi ambazo ni ya Magufuli na Samia zilizopo Area C jijini hapa.

Mkurugenzi huyo alisema teknolojia hiyo ni nzuri kwa kuwa ni rafiki kwa mazingira, ni rahisi na gharama zake ni ndogo hivyo aliishauri serikali kuitumia katika ujenzi wa barabara zake.



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa jengo eneo la katikati ya Jiji la Dodoma jana. Tangu serikali kuhamishia makao makuu yake jijini humo, uwekezaji wa majengo makubwa umekuwa ukifanyika kwa kasi kubwa zaidi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wizara yaingia mkataba utafiti wa mboga

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WIZARA ya Kilimo imeingia mkataba wa miaka 10 na Kampuni ya AVRDC The World Vegitable Center ya Tengeru mkoani Arusha, ili kufanya utafiti wa mbegu bora za kilimo cha mbogamboga na kuinua sekta hiyo.

Imesema lengo la kufanya hivyo ni kutaka sekta hiyo ichangie pato la taifa kwa kiwango kikubwa kama zilivyo sekta nyingine.

Katika hafla ya utiaji saini mkataba huo juzi, Katibu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, alisema ameagiza ziundwe kamati ndogo kwa ajili kusimamia mpango huo.

Alisema kutokana na hatua hiyo, serikali itakwenda kusimamia utafiti huo ili kuimarisha mpango huo ambao una malengo mazuri.

Alisema pia wanakwenda kuimarisha vyuo vya kilimo pamoja na taasisi nyingine zilizochini ya TARI, ili kusaidia kukuza mpango huo.

Mtendaji huyo wa wizara alisema serikali iko mstari wa mbele kwa ajili ya kuinua kilimo cha mbogamboga ambacho hivi sasa kipo juu kimauzo nchini.

"Serikali imejipanga kuinua kilimo cha mbogamboga, tunaomba kamati zitakazoundwa zikafanye kazi," aliagiza Kusaya.

Alisema ARVDC imefanya jambo zuri, hivyo serikali kwa kushirikiana na kampuni hiyo watasimama imara kwa ajili ya kutekeleza.

Mkurugenzi AVRDC Kanda ya Afrika Mashariki na Kati, Dk. Gabriel Lugalema, alisema jukumu lao ni kukusanya, kuchakata na kutunza mbegu bora na kutoa wataalamu.

Dk. Lugalema alisema mwaka 2008 hadi 2018, wamefanikiwa kutoa wataalamu 400, toka nje ya nchi na wengine 2,000 toka maeneo mbalimbali nchini.

Alisema lengo lao ni kuona watu wananufaika na kilimo hicho ambacho kinalimwa na watu wengi katika maeneo mbalimbali nchini.



HABARI MBEYA

# Anaswa tuhuma za rushwa mkutano kura za maoni CCM

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Mbeya, inamshikilia Paschal Mwakyusa, mkazi wa Kyela mkoani hapa kwa tuhuma za kugawa rushwa kwa baadhi ya wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilayani humo.

Kwa mujibu wa taarifa ya taasisi hiyo iliyotumwa kwa vyombo vya habari jana na Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Mbeya, Julieth Matechi, Mwakyusa alikamatwa juzi saa 5:00 asubuhi wakati wa mkutano wa kupiga kura za maoni za ubunge katika jimbo hilo.

Alisema baada ya uchunguzi, walibaini kuwa mtuhumiwa ni mpambe wa aliyekuwa mtia nia wa nafasi ya ubunge wa jimbo hilo, Hanter Mwakifuna, na kwamba alikuwa anagawa rushwa hiyo kwa ajili ya kuwashawishi wajumbe kumpigia kura.

**Kwa mujibu wa kifungu namba 15 cha Sheria ya TAKUKURU ya mwaka 2007, ni kosa kwa mtu yeyote kutoa ama kupokea rushwa na vitendo hivyo vinatafsiriwa kuwa ni kosa la jinai kwa mujibu wa sheria hiyo.**

"Mtuhumiwa alipopekuliwa, alikutwa na Sh. milioni 1.78. Uchunguzi bado unaendelea juu ya tukio hilo na mtuhumiwa yuko mahabusu akisubiri uchunguzi. Baada ya hapo hatua zaidi za kisheria zitachukuliwa dhidi yake," alisema Matechi.

Aliwashukuru wananchi wa Kyela waliotoa taarifa za siri kuhusu tukio hilo, taarifa ambazo ziliwasaidia maofisa wa TAKUKURU wilaya kumtia nguvuni Mwakyusa. Matechi aliwataka wananchi wa maeneo yote ya mkoa wa Mbeya kuendelea kushirikiana na TAKUKURU pamoja na vyombo vingine vinavyoshiriki mapambano dhidi ya rushwa, ili kukomesha vitendo hivyo na kufanya uchaguzi wa haki.

Alisema taasisi hiyo inaendelea kufuatilia taarifa mbalimbali ambazo wananchi wanaipenyezea ili kujua ukweli wake na kama ni kweli, wahusika wachukuliwe hatua zinazostahili kwa mujibu wa sheria za nchi.

Matechi alisema taasisi hiyo pia inaendelea kufuatilia michakato ya uchaguzi kwenye vyama mbalimbali vya siasa, ili kuhakikisha hakuna mianya ya rushwa inayoruhusu wagombea kuwahonga wapigakura wao.

"Kwa mujibu wa kifungu namba 15 cha Sheria ya TAKUKURU ya mwaka 2007, ni kosa kwa mtu yeyote kutoa ama kupokea rushwa na vitendo hivyo vinatafsiriwa kuwa ni kosa la jinai kwa mujibu wa sheria hiyo," alisisitiza Matechi.

Pia aliwataka viongozi wa vyama vya siasa kushirikiana na taasisi hiyo kukabiliana na vitendo vya rushwa kwenye mchakato wa uchaguzi wa ndani ya vyama kwa kuepuka kushiriki vitendo hivyo na kutoa taarifa za watu wanaoshiriki.

Sambamba na hilo, aliwataka wananchi na wajumbe wa mikutano mikuu ya vyama vya siasa kutowachagua wagombea ambao wanawahonga wapiga kura ili wawachaguwe.

Tangu mchakato wa uchaguzi wa ndani ya vyama vya siasa, TAKUKURU Mkoa wa Mbeya, imewanasa viongozi watatu wa Chama Cha Mapinduzi wakidaiwa kuwahonga wapigakura.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Prof. Sifuni Mchome (katikati), akifungua mafunzo ya utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria kwa watoto walio kwenye vituo vya Polisi na Magereza, kwa maofisa wa Jeshi la Polisi wa Mikoa ya Mbeya na Iringa jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wanaokiuka kanuni waonywa kukatwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Mbeya Mjini kimewatahadharisha watia nia wa nafasi za udiwani wa kata mbalimbali za wilaya hiyo, kuwa wataondolewa kwenye mchakato endapo watabainika kukiuka kanuni za chama hicho.

Tahadhari hiyo ilitolewa juzi na Mwenyekiti wa Chama hicho, Afrey Msomba, kwenye Mkutano Mkuu wa CCM wilaya wa kupiga kura za maoni kwa ajili ya kumpata mtu atakayepeperusha bendera ya chama hicho kwenye nafasi ya ubunge katika uchaguzi mkuu wa Oktoba, mwaka huu.

Alisema moja ya vitendo ambavyo vinaweza kusababisha mtiania kuondolewa kwenye mchakato ni kubainika akishiriki vitendo vya rushwa ambavyo ni kinyume cha sheria za nchi.

"Tunataka kuwapata wagombea ambao ni wasafi na watauzika. Lengo la chama chetu ni kushinda kwenye kata zote 36 na kuiongoza Halmashauri ya Jiji letu ambalo lilikuwa chini ya wapinzani," alisema Msomba.

Alisema katika kura za maoni za madiwani, chama hicho kimewaongeza mabalozi kuwa wajumbe wa mkutano mkuu wa kata na kwamba nao watashiriki kwenye kupiga kura za maoni mwaka huu.

Awali, Katibu wa CCM Wilaya ya Mbeya Mjini, Gervas Ndaki, alisema baada ya kura za maoni za ubunge wameanza maandalizi kwa ajili ya kura za maoni za madiwani.

Alisema michakato yote inafanyika kwa uwazi na kwamba kura zinahesabika hadharani kama Halmashauri Kuu ya CCM ilivyofanya jijini Dodoma kuwapata wagombea urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mgombea urais wa Zanzibar.

## Polisi yapewa somo kupunguza kesi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Prof. Sifuni Mchome, amewataka askari polisi kutumia sheria kufifisha baadhi ya makosa na kufanya upatanishi kwa wananchi wanaokinzana na sheria.

Katika kufanya hivyo, badala ya kila kosa la jinai kulipeleka mahakamani, lipatiwe ufumbuzi kabla ya hatua hiyo.

Prof. Mchome alisema hayo jana jijini hapa wakati akifungua mafunzo ya siku mbili kwa askari wa jeshi hilo, kutoka mikoa ya Mbeya na Iringa kuhusu utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria kwa watoto wanaokinzana na sheria. Alisema mwaka 2017 serikali ilitunga sheria inayoruhusu askari wa Jeshi la Polisi kufifisha baadhi ya makosa yanayofifishika na kufanya upatanishi kwa wananchi wanaosigana kabla ya kuwafikisha mahakamani.

Lengo la sheria hiyo, kwa mujibu wa Prof. Mchome, ni kupunguza msongamano wa kesi mahakamani na kuondoa mrundikano wa wafungwa na mahabusu magerezani.

Pia aliwata askari wanaopewa mafunzo hayo kuwa mabalozi kwa kuonyesha mfano wa kutumia njia hiyo ambayo ipo kwa mujibu wa sheria na kuwahimiza wenzao kutekeleza kifungu hicho cha sheria.

Mratibu wa Mafunzo hayo, Giffrin Mwakapuje, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo askari wa jeshi hilo katika mikoa ya Mbeya na Iringa kushughulikia masuala ya jinai yanayowahusu watoto kwa haki.

Alisema wizara inaamini kuwa polisi wanao uwezo wa kuwasaidia watoto hasa wanaokinzana na sheria kupata haki na pia kupunguza vitendo vya ukatili wanavyofanyiwa watoto.

Baadhi ya askari wanaoshiriki mafunzo hayo, walisema yatawasaidia kukabiliana na changamoto wanazokutana nazo wakati wanapopata kesi zinazowahusu watoto

Mmoja wa askari hao, Bihem Mayengela kutoka katika Kituo cha Polisi Kyela, alisema miongoni mwa visababishi vya watoto kuingia kwenye matatizo ya kukinzana na sheria ni pamoja na kutotimiziwa mahitaji na walezi au wazazi wao.

"Kwa mfano, mtoto anaweza kuwa na mahitaji ya madaftari ya shule na akayakosa kwa wazazi au walezi wake, hivyo akaamua kwenda kudokoa fedha mahali ili akidhi mahitaji yake na kujikuta kwenye matatizo. Hii inakuwa imesababishwa na wazazi kushindwa kumtimizia mahitaji yake ndiyo sababu mtoto huyo akajikuta anakinzana na sheria," alisema Mayengela.





# Ofisa usalama feki atiwa mbaroni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JESHI la Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, linamshikilia John Samwel Manga (32), kwa kujifanya ofisa usalama wa taifa na kuwatapeli wananchi.

Akitoa taarifa kwa waandishi wa habari mwisho wa wiki, Kamanda wa Polisi wa mkoa huo, Awadhi Juma Haji, alisema kijana huyo mkazi wa Fuoni Unguja, aligundulika baada ya jeshi hilo kumfuatilia matukio aliyokua akiyafanya kwa watu mbalimbali kwa kuwadanganya atawasaidia kuwapatia ajira katika idara ya usalama wa taifa na idara zingine.

Alisema mtuhumiwa huyo alikuwa akichukua fedha na vitu tofauti kwa kisingizio cha kuwapatia ajira hizo.

Alisema mtuhumiwa huyo alifanikiwa kumtapeli Asha Omar Hamdan, Sh. 500,000 kwa kumwambia kuwa atamsaidia kupata ajira katika idara ya usalama wa taifa.

Pia, alisema anadaiwa kumtapeli Abubakar Ali, Sh. 2,590,000, kompyuta moja mpakato na kamera.

Alisema kuwa katika uchunguzi wamefanikiwa kupata nyaraka mbalimbali ikiwamo vyeti vya kumaliza masomo vya watu mbalimbali, vyeti vya kuzaliwa, na viapo vya mahakama.

Alieleza kuwa vitu vingine alivyokamatwa navyo ni kamera na picha mbalimbali za baadhi ya watu aliowafanyia utapeli.

**Mtuhumiwa huyo alifanikiwa kumtapeli Asha Omar Hamdan, Sh. 500,000 kwa kumwambia kuwa atamsaidia kupata ajira katika idara ya usalama wa taifa.**

# Kampuni zashauriwa kujenga hoteli za kitalii

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar Balozi Seif Ali Iddi, amezishauri kampuni za uwekezaji katika sekta ya biashara kuangalia uwezekano wa kujenga hoteli ya kitalii katika Uwanja wa Ndege wa Pemba kwa lengo la kutoa huduma kwa wasafiri na wananchi wanaotumia uwanja huo.

Alisema mfumo wa huduma za hoteli unaokuwapo katika viwanja mbalimbali vya ndege duniani hulenga kuwaondolea usumbufu wasafiri wa anga kuzitafuta huduma hizo maeneo ya mijini kwa vile baadhi ya viwanja hivyo huwapo nje ya miji.

Balozi Seif Ali Iddi aliyasema hayo alipofanya ziara fupi ya kukagua maendeleo ya mradi wa ujenzi wa hoteli ya kimataifa ya Golden Tulip Airport iliyopo pembezoni mwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Aman Karume ulio chini ya Kampuni ya Royal Group.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia taasisi zake za uwekezaji ina nia ya kuona fursa ya ujenzi wa hoteli ya kitalii katika Uwanja wa Ndege wa Pemba inachangamkiwa na wafanyabiashara wenye uwezo kwa kuanzisha mradi huo muhimu unaoweza kutoa huduma na ajira kwa vijana.

**Nimejiunga na ADATADEA kwa matarajio yangu makubwa viongozi wetu watafanya siasa za kistaarabu zitakazowaunganisha wananchi wa Unguja na Pemba.**

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, aliupongeza uongozi wa Kampuni ya Royal Group kwa uamuzi wake wa kuanzisha mradi huo mkubwa utakaosaidia kuongeza pato la taifa, huduma kwa wasafiri na kwa upande mwingine ajira kwa wananchi wazalendo.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Royal Group, Hassan Mohammed Raza, alisema ujenzi huo unaotarajiwa kuchukua miezi 16 utakamilika mwezi Oktoba, mwaka huu.

Hassan alisema ujenzi wa jengo hilo litakalokuwa na vyumba 62 vya kulala, eneo la kuegesha magari 150 kwa wakati mmoja linatarajiwa kugharimu jumla ya Dola za Kimarekani milioni 7.5 sawa na zaidi ya Sh. bilioni 17.1.

Mkurugenzi huyo alieleza kwamba pamoja na mambo mengine uongozi wa Royal group umezingatia huduma za michezo kwa kuweka bwawa maalum la kuogelea pamoja na sehemu za mazoezi kwa wasafiri wanamichezo.

Alisema mradi huo utakapokamilika utatoa huduma kwa wasafiri wa anga wanaotumia uwanja huo kwa kuzingatia umuhimu wa usalama wa abiria unaokwenda sambamba na vile vigezo vya viwanja vya ndege vya kimataifa.

Naye Meneja wa Operesheni wa uwanja huo, Haji Haji alisema vifaa maalum vitawekwa katika hoteli hiyo vitakavyosimamiwa na watendaji wa taasisi zote zinazohusika na masuala ya uwanja wa ndege katika kuona msafiri anapata huduma zinazostahiki.

Haji alisema usafiri wa mabasi utawekwa kwa ajili ya kuwahudumia abiria wanaokuwamo ndani ya hoteli hiyo na kuwafikisha kwenye mlango na ndege wanazosafiria.



Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM Taifa ambaye ni Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Jimbo la Mahonda, akipigakura ya maoni kuwapendekeza wanachama watakaochaguliwa kuwania nafasi ya uwakilishi na ubunge kwenye uchaguzi mkuu ujao, katika ukumbi wa CCM Mkoa Mahonda, jana. **PICHA: OMPR – ZNZ**

# Ujenzi maabara za shule kuibua wanasayansi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Katibu Mkuu Utawala na Uendeshaji, Mwalimu Abdullah Mzee Abdullah, amesema kukamilika kwa maabara na shule za kisasa kutaifanya Zanzibar kuwa chimbuko la wanasayansi.

Akizungumza jana katika ziara ya kuangalia majengo mbalimbali ya maabara za kisayansi, alisema ujenzi wa maabara hizo ni kuhakikisha nchi inazalisha wataalamu wazalendo wa kuacha kutegemea wataalamu kutoka nje ya nchi.

Abdullah alisema ni harakati za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuhakikisha kila mwanafunzi anapata huduma bora ya elimu na bure pamoja na kuwa miundombinu mizuri yenye mahitaji kamili na imara.

Alisema sasa ni muda wa wanafunzi kufanya vizuri katika masomo yao kwa kuwa serikali kupitia Wizara ya Elimu inajitahidi kujenga majengo yenye kuzingatia mahitaji ya watu wote.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Mipango sera wa wizara hiyo, Khalid Masoud Waziri, aliwataka makandarasi wa majengo hayo kuhakikisha wanamaliza matengenezo madogo madogo yaliopo ili yaweze kuwa katika hali ya ubora zaidi.

Alisema kukamilika kwa majengo hayo ni ushirikiano baina ya watendaji wa Wizara ya Elimu kupitia kitengo cha ujenzi na thamani pamoja na makandarasi ili kuhakikisha majengo yanakua na kiwango kilichokusudiwa.

Kwa upande wake Mshauri Elekezi wa ujenzi wa mradi huo, Arch Casmil Ntobangi, aliiomba Wizara ya Elimu kuwapatia muda wa wiki moja ili kuhakikisha wanaweka sawa matengenezo madogo madogo yaliobaki.

Katika ziara hiyo walikagua maabara ya Sayansi ya Kisauni, Jang'ombe na Mwanakwerekwe na wizara ilisaini fomu ya makabidhiano ya majengo hayo na Kampuni ya ujenzi CRJE kutoka nchini China, baada ya kuridhishwa na ujenzi huo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL,** Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile: **Kuboresha biashara, Kulipa kodi ya nyumba, Kumalizia tenda, Kulipa ada, Kulipa matibabu n.k.**
**Mawasiliano** yetu **Dar es salaam** – 0768 928 516. **Arusha** – 0677 226 960.

## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



THOMAS DOTTO MGAYWA anatangaza kupotea kwa cheti kidato cha nne chenye index namba S.0989/0070 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia KIBAHA HIGH SCHOOL mwaka 2016.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
DAR/URA/RB/459667/2020.

158187

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FOMU II**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya PONGWE - TANGA**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 18/2020**

**Ombi la SAUM ABDALLAH kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu ZINDUNA ISSA SHEREHE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 23/07/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo .

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.
Tarehe 03/07/2020.

PUNGWE

215819902

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**HATI YA KIAPO**

Mimi KHAMIS MWADINI HAJI wa S.L.P TANGA, nikiwa na akili timamu nimefika mbele ya Hakimu/Wakili na kutamka yafuatayo:

1. Kwamba mimi ni mmiliki wa kiwanja Na. 52 kitalu "Q" Msambweni – Mabawa Tanga.
2. Kwamba, kiwanja hicho nimekimiliki kwa muda mrefu sasa.
3. Kwamba, Hati hiyo ya kiwanja imepotea na nimefanya jitihada za kuitafuta bila mafanikio.
4. Kwamba, kwa kiapo hiki ifahamike kwa mtu/taasisi yeyote kuwa hati ya kiwanja imepotea.
5. Kwamba, nawasilisha taarifa hii ya upotevu kwenye mamlaka ya Jeshi la Polisi nikiomba hati ya upotevu wake (Loss Report).

**UTHIBITISHO**
Nathibitisha kuwa yote niliyoyatamka hapo juu ni kweli , kweli tupu kwa kadri nijuavyo kwa sharia ya viapo.

RESIDENT MAGISTRATE TANGA

Muapaji

158196

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RAMADHANI SALUM MWIKALO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya PRADO yenye namba ya usajili T316-AWJ iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochocte cha Polisi.

Polisi Taarifa:
DOD/DOD/RB/443197/2020

158189

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RAZAK ISMAIL** MCHIKA anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 187 AFW. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
MTW/MTW/R-B/527954/2020.

158188

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**Probate and Administration Cause No. 45 of 2020**

**In the matter of the estate of the late MAGRETH THOMAS MBENYETI**
**Of Kikuyu within Dodoma City**
**And**
**In the matter of application for letters of administration by WILFRED R. MAKUNDI**

**GENERAL CITATION**

**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner. Objections to the grant should be filed on or before the 29 day of 7, 2020.
**Dated at Dodoma this 17 day of 7, 2020.**

RESIDENT MAGISTRATE DODOMA DISTRICT
RESIDENT MAGISTRATE

215819202

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**Probate and Administration Cause No. 46 of 2020**

**In the matter of the estate of the late ALEX MWANANCHI MNEMELE**
**Of Kikuyu within Dodoma City**
**And**
**In the matter of application for letters of administration by VERONICA ALEX MNEMELE**

**GENERAL CITATION**

**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner. Objections to the grant should be filed on or before the 7 day of 8, 2020.
Dated at Dodoma this 21 day of July, 2020.

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE DODOMA DISTRICT

215819102

---


***Uza, Chenye Thamani Kubwa***

***Kwa Kutangaza Nasi***

***Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***



**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

**HABARI KIMATAIFA**

# Trump kutumia jeshi kuzima maandamano

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Donald Trump, ametishia kutuma maofisa wa jeshi katika miji mingi zaidi Marekani kudhibiti maandamano yanayoendelea.

Rais Trump mwanzoni mwa wiki alikosoa miji kadhaa inayoongozwa na Chama cha 'Liberal Democrats', ikiwamo Chicago na New York, akisema kuwa viongozi wanaogopa kuchukua hatua. Alisema kuwa maofisa waliotumwa Oregon wamefanya kazi nzuri ya kurejesha amani.

Hata hivyo, maofisa wa eneo walisema kuwa maofisa wa serikali wanafanya hali kuwa mbaya zaidi.

Viongozi wa majimbo walitaka Rais Trump kuondoa maofisa alioagiza kupelekwa huko Portland na kumshutumu kwa kufanya hali kuwa mbaya zaidi kama njia ya kutafuta ushawishi wa kisiasa mwaka wa uchaguzi.

Akizungumza katika Ikulu ya Marekani, Rais Trump alirejelea wito wa utekelezaji sheria na utaratibu.

"Tunatuma vikosi, hatuwezi kuacha hili liendelee kutokea katika miji, hatuwezi kuacha hili litokee katika nchi yetu, yote ni maeneo yanayoongozwa na Chama cha Liberal Democrats," alisema Rais Trump.

**Tunatuma vikosi, hatuwezi kuacha hili liendelee kutokea katika miji, hatuwezi kuacha hili litokee katika nchi yetu, yote ni maeneo yanay-oongozwa na Chama cha Liberal Democrats.**

Aliongeza: "Maofisa wa serikali wamekuwa hapo kwa siku tatu na wamefanya kazi nzuri kwa kipindi fupi tu, hakuna matatizo. Wanashika watu wengi na kuwafunga viongozi gerezani. Hao ni watu wanaoasi serikali."

Alitaja miji ya New York, Chicago, Philadelphia, Detroit, Baltimore na Oakland akiwa anazungumzia matatizo yatokanayo na ghasia.

Rais Trump pia alipongeza juhudi za maofisa hao waliosababisha utata kwa kutekeleza sheria huko Portland. Mji huo umekuwa ukishuhudia maandamano dhidi ya unyama unaotekelezwa na polisi mjini humo tangu kutokea kwa mauaji ya George Floyd, mwanaume mweusi huko Minnesota Mei.

Rais Trump alituma maofisa wa serikali katika hilo la magharibi mwa pwani ya Marekani wiki mbili zilizopita kutuliza maandamano hayo.

Baadhi ya maofisa wametumia magari ya kawaida na kusababisha ukosoaji mkubwa kutoka kwa Democrats na wanaharakati.

Wiki iliyopita, wasiwasi kati ya waandamanaji na maofisa hao wa polisi umeongezeka na viongozi wa eneo wametoa wito kuwa maofisa hao wa serikali kuu waondoke mjini humo.

Rais Trump alisema kuwa gavana wa Oregon, meya wa Portland na viongozi wengine wa majimbo wanaogopa raia hao aliowataja kama wanaopinga serikali.

Maofisa hao ni sehemu ya idara mpya ya usalama wa ndani.

Wamepelekwa katika eneo hilo kwa agizo la Rais Trump la kulinda masanamu, lililotiwa saini na Rais Trump mwezi uliopita.

Agizo hilo linaruhusu maofisa wa serikali kupelekwa sehemu yoyote bila viongozi wa eneo kuombwa ruhusa ya kufanya hivyo.

Pia maofisa 150 wamepangiwa kupelekwa Chicago wiki hii, ili kusaidia maofisa wengine wa serikali pamoja na polisi wa Chicago kupambana na uhalifu.

Meya wa Chicago, Lori Lightfoot, awali alisema ana wasiwasi kwa hatua ya Rais Trump ya kupeleka maofisa wa serikali mjini humo.

Akizungumza na kituo cha habari cha CNN Jumapili, Meya wa Portland, Ted Wheeler, alisema: "Kuna wanajeshi kadhaa ikiwa siyo mamia mjini humo, uwepo wao unafanya kuwe na maandamano na uharibifu zaidi wa mali. Hatujawaomba kuja hapa. Na hasa tunachotaka ni wao waondoke," alisema Wheeler. **BBC**



Viongozi wa mataifa ya Jumuiya ya Ulaya (EU) wakiwa katika kikao cha pamoja cha kupitisha bajeti ya kukabiliana na athari zilizotokana na ugonjwa wa virusi vya corona. **PICHA: REUTERS**

## Nchi za Umoja wa Ulaya zakubaliana kufufua uchumi

**BRUSSELS,** Ubelgiji

HATIMAYE viongozi wa Umoja wa Ulaya (EU), wamekubaliana namna ya kugawana zaidi ya Euro bilioni 750 kuisaidia katika uimarishwaji wa uchumi wa nchi zao.

Baada ya mazungumzo ya siku nne, viongozi wa nchi za EU walikuwa wakikutana kwa mazungumzo jijini Brussels hatimaye wamefikia mkataba, kuhusu mpango wa kunusuru uchumi baada ya janga la corona.

Viongozi hao kutoka nchi 27 wamefikia mkataba jijini Brussels jana kuhusu mpango wa kihistoria wa kunusuru uchumi baada ya janga la corona.

Rais wa Baraza la Umoja wa Ulaya, Charles Michel, ndiye aliyetangaza kwenye ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Twitter.

Naye Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron, kwenye ukurasa huo alisema: "Siku ya kihistoria kwa Umoja wa Ulaya".

Pia alimpongeza Rais Macron kwenye ukurasa wake wa Twitter, sekunde chache baada ya kutangazwa mkataba huo.

Mkutano huo uliowakutanisha viongozi wote wa nchi wanachama wa EU ambao awali ulipangwa kufanyika saa 10:00 alasiri uliahirishwa mara nyingi ili kuzingatia mahitaji ya kila mmoja. Na ulianza kabla ya saa 9:30 usiku.

Miongoni mwa makubaliano yaliyofikiwa ni pamoja na Euro Bilioni 390 kutolewa kama misaada kinyume na Euro bilioni 500 iliyokuwa imetangazwa hapo awali.

Rais wa Halmashauri Kuu ya EU, Ursula Von der Leyen alionyesha furaha kutokana na kuwa makubaliano ya mwaka huu hayakuwa baina ya nchi na nchi ila mataifa yameonyesha imani yake kwa halmashauri hiyo kuu.

Von der Leyen alisema kuwa viongozi wanadhamiria kuleta mageuzi na uwekezaji zaidi Ulaya.

Alisema: "Ninafurahi kwamba tumeweza kuyapata makubaliano haya na kufufuka kwa ulaya kutakuwa kijani. Bajeti hii mpya itayapa nguvu makubaliano ya kijani ya ulaya, itaongeza kasi ya uchumi wa ulaya kuwa wa kidijitali na mageuzi ya kitaifa yataongezwa. Tunawekeza kwa mustakabali wa ulaya". **RFI**

# Rais Kenyatta aitisha kikao kuikabili corona

**NAIROBI,** Kenya

RAIS wa Kenya, Uhuru Kenyatta, ameitisha kikao maalumu cha kilele na magavana kufuatia ongezeko la visa vya ugonjwa wa corona.

Taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari, Rais Kenyatta alisema kikao hicho kitatathmini utayarifu wa majimbo kukabiliana na virusi hivyo.

Taarifa hiyo imesema kuwa, kwenye kikao hicho wataangalia mbinu za matibabu ya ugonjwa huo na namna ugonjwa huo utakavyokuwa umesambaa katika miezi ya Agosti na Septemba.

Jimbo la Tana River limekuwa jimbo la karibuni zaidi kuripoti kisa cha virusi hivyo na kuongeza idadi ya majimbo yenye visa hivyo kuwa 44 kati ya 47.

Waziri wa Afya, Mutahi Kagwe, alieleza wasiwasi kuhusu kuongezeka kwa visa hivyo kila siku.

Kenya imerekodi jumla ya visa 13,770 mpaka sasa, baada ya visa vingine 400 kuripotiwa Jumatatu. Na katika hatua nyingine soko la maua nchini humo limeanza kupata uhuru kwa kiwango cha asilimia 85 katika kipindi hiki ambacho soko la Ulaya linafunguliwa baada ya vizuizi vya kukabiliana na janga la corona.

Taarifa ya sekta hiyo muhimu ya kibiashara ilionyesha kuwa Kenya itaingia katika mwendelezo kamili wa ufanyaji biashara kwa mwaka ujao.

Wakulima wa Kenya walilazimika kuitelekeza shehena ya maua yao baada ya mataifa mengi ya ulaya kufunga mipaka yao Machi, mwaka huu na wakazi kuwekewa masharti katika shughuli za mazishi na harusi. **DW**

# BALE HAONDOKI MADRID – WAKALA




**MARID,** Hispania

GARETH Bale "haendi kokote" wakati uvumi ukisambaa kuhusu majaliwa yake pale Real Madrid, kwa mujibu wa wakala wake, Jonathan Barnett.

Bale amejikuta yeye mwenyewe nje ya kikosi cha Madrid ambao walipiku wapinzani wao Barcelona na kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, msimu huu, amecheza mechi mbili tu tangu kurudi kwa msimu huu 2019-20 baada ya kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Fowadi huyo ambaye tabia yake imekuwa ikishutumiwa, amecheza mechi 16 tu za Ligi Kuu msimu huu na aliachwa na kocha Zinedine Zidane katika kikosi kilichocheza mchezo wa mwisho wa ligi dhidi ya Leganes, Jumapili iliyopita.

Licha ya kutokuwa na nafasi kwenye kikosi hicho, Barnett amesisitiza mteja wake Bale hana mpango wa kuondoka pale Santiago Bernabeu.

"Gareth yuko vizuri. Ana miaka miwili imebaki kwenye mkataba wake," alisema akiiambia BBC Sport. "Anapenda kuishi Madrid na haendi kokote.

"Bado ni mzuri kama mtu yoyote ndani ya timu. Ni juu ya Zinedine Zidane.

"Bila shaka kumekuwa na timu zinazomwania, lakini ni ngumu klabu duniani kumtimizia kile anachokitaka."

Bale alifurahia mafanikio tangu alipojiunga na Madrid akitokea Tottenham mwaka 2013, akifunga mabao zaidi ya 100 na kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mara nne pamoja na LaLiga.

# Sarri kubakia Juventus msimu ujao




**TURIN,** Italia

MKURUGENZI wa Juventus, Fabio Paratici, amesema "bila shaka" Maurizio Sarri ataendelea kuwa kocha mkuu wa miamba hao wa Serie A kwa msimu ujao wa 2020/21.

Juve wapo kwenye nafasi nzuri ya kushinda taji la Ligi Kuu Italia, Scudetto, kwa mara ya tisa mfululizo, lakini Sarri ameendelea kuhusishwa na mpango wa kuondoka hapo baada ya kutua akitokea Chelsea mwanzoni mwa msimu huu.

Sarri ameibua uvumi mara kadhaa kwamba atafukuzwa mwishoni wa msimu huu hata kama ataiwezesha Juventus kubeba taji la Serie A, huku kocha wa zamani wa Tottenham, Mauricio Pochettino akihusishwa kupewa nafasi hiyo.

Hata hivyo, Paratici alimwagiwa maji ya baridi kuhusu uvumi huo Jumatatu wakati wakishinda 2-1 dhidi ya Lazio, ushindi ulioipeleka Juve kuwa na pointi nane zaidi kileleni mwa msimamo huku zikiwa zimesalia mechi nne ligi kumalizika.

"Mazungumzo yote yapo kwenye vyombo vya habari. Nimekuwa hapa kwa miaka 10, tumekuwa juu ya msimamo kwa mara ya tisa mfululizo," amesema Paratici akiiambia Sky Sport Italia.

"Tulishinda mataji na Max Allegri kwa miaka mitano, bado kila wakati hata baada ya ushindi kulikuwa na uvumi.

"Bila shaka, Sarri atakuwa kocha wa Juventus msimu ujao."

Sarri yupo kwenye nafasi ya kushinda taji lake la kwanza la ligi akiwa kocha, awali akiwa ameshinda taji la Ligi ya Europa akiwa na Chelsea msimu uliopita.

## Guardiola kutopumzisha wachezaji Man City

**MANCHSTER,** England

PEP Guardiola hatawapa muda wa kumpumzika Manchester City wakati wowote baada ya kumalizika kwa msimu wa Ligi Kuu England ili waendelee kujifua kwa ajili ya mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Real Madrid.

City bado ina nafasi ya kuongeza taji la Ulaya baada ya kutwaa lile la EFL msimu huu licha ya kutolewa na Arsenal kwenye nusu fainali ya FA, wakichapwa 2-0.

Guardiola alishutumu kiwango cha wachezaji wake katika dakika 45 za mwanzo na amepanga kutowapa muda wa kupumzika kwa siku 12 na kuendelea kujifua pale Etihad kuelekea mchezo wa mwisho wa Ligi Kuu dhidi ya Norwich City Julai 26 na Madrid Agosti 7, mwaka huu.

City wanaongoza kwa ushindi wa 2-1 katika mchezo wa kwanza uliopigwa uwanja wa Santiago Bernabeu, Februari na jana Jumanne walikuwa wakicheza mchezo wa ligi dhidi ya Watford, na Guardiola amekataa uwezekano wa kuwapumzisha wachezaji.

"Hapana, hapana, hapana, baada ya mchezo dhidi ya Watford tutaendelea kujifua kwa mazoezi kwa wiki mbili," amesema Guardiola, ambaye timu yake ina uhakika wa kumaliza kwenye nafasi ya pili nyuma ya Liverpool.

"Tunakwenda kucheza mechi mbili zinazofuata. Nitajaribu kuwaacha wote wacheze. Tutaona nini kitatokea."



# Arteta: Xhaka ni mfano mzuri kwa Ozil, Guendouzi

**LONDON,** England

MESUT Ozil na Matteo Guendouzi wanatakiwa kufuata mfano wa Granit Xhaka kama wanataka kuendelea kupata nafasi ya kucheza Arsenal, Mikel Arteta amesema.

Wawili hao, Ozil na Guendouzi wamekuwa wakiachwa nje ya dimba wakati Arsenal wakifurahia "kufufuka" kwa kiwango chao chini ya Arteta, ambaye ameiongoza klabu hiyo kushinda mechi sita kati ya nane zilizopita.

Ukiwamo ushindi dhidi ya mabingwa wa Ligi Kuu England Liverpool na Manchester City kwenye nusu fainali ya Kombe la FA wiki iliyopita, huku Xhaka akionyesha kiwango cha kuvutia katika mechi zote mbili.

Ni tofauti na mwanzoni mwa Novemba, miezi miwili kabla ya Arteta kutua hapo kama kocha mkuu,wakati majaliwa ya Xhaka kwenye dimba la Emirates yalionekana kufikia mwisho.

"Changamoto ya Granit ilikuwa ni kumshawishi yeye kwamba bado kulikuwa na nafasi kwa ajili yake, hapa nilikuwa na imani kubwa nae na hilo likabadilisha mambo kwa haraka sana," alieleza Arteta kwa waandishi wa habari kuelekea mchezo wa Ligi Kuu England dhidi ya Aston Villa ambao ulichezwa jana usiku.

"Alitakiwa kupeleka ujumbe sahihi. Jambo la kwanza alikubali kujiamini na kwamba angeweza kufanya chochote uwanjani, na sisi tukampa sapoti.

"Kwa hakika kabisa nafurahia kuona namna mashabiki wanavyomshangilia na kumpa sapoti, nafikiri sasa wamekubali kwamba anaweza kufanya makubwa kwa klabu. Hayo yamepita na sasa ana mtazamo chanya kabisa kwa sababu alijifunza wakati akipitia magumu.

Ozil hajajumuishwa kwenye kikosi tangu Machi, kabla ya mashindano kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, huku kiungo Guendouzi hajawa kwenye jezi ya Arsenal tangu kwenye mchezo wa Brighton and Hove Albion wakati wakichapwa 2-1 Juni 20, mwaka huu.




# ANELKA: SALAH, MANE MSIENDE REAL MADRID



**LIVERPOOL** England

MOHAMED Salah na Sadio Mane wanatosha kuichezea Real Madrid katika macho ya Nicolas Anelka, ingawa Mfaransa huyo amewashauri wawili hao kubakia Liverpool.

Washambuliaji hao, Salah na Mane wamekuwa nguzo muhimu ya mafanikio kwa wekundu hao wa Anfield msimu huu wakati wakitwaa taji la Ligi Kuu England kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka 30.

Salah amefunga mara 19 kwenye Ligi Kuu England msimu huu na kutoa pasi za mwisho tisa, huku Mane amezidiwa mabao mawili tu, wakati wawili hao wakicheza kwa ushirikiano mzuri kutoka kwa straika wa kati Roberto Firmino.

Mafanikio hayo yamefanya klabu kama Real Madrid kuonyesha nia ya kuwataka, lakini Anelka, ambaye alicheza kwa Los Blancos hao msimu wa 1999-00 baada ya mafanikio makubwa kwenye Ligi Kuu England akiwa na Arsenal, anahisi Liverpool ni sehemu bora zaidi kwa wawili hao, Salah na Mane.

"Ni safu ya watatu inayofurahisha pale mbele," alisema Anelka akiiambia televisheni ya Liverpool.

"Nawapenda wao, hasa Roberto Firmino kwa sababu ndio nguzo ya mafanikio ya Mohamed Salah na Sadio Mane.

"Salah na Mane wapo kwenye orodha ya wachezaji bora watano duniani kwa sasa. Wana ubora wa kuichezea Real Madrid.

# *Cazorla amfuata Xavi Al Sadd*

**DOHA,** QATAR

SANTI Cazorla amekubali kujiunga na klabu ya Al Sadd baada ya kumaliza mkataba wake pale Villarreal.

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 35 sasa amekwenda Doha kukamilisha taratibu za mikataba kabla ya kujiunga rasmi na timu hiyo inayonolewa na mchezaji mwenzake wa zamani kwenye Timu ya Taifa ya Hispania, Xavi, ambapo walishinda kwa pamoja taji la Ulaya mara mbili.

Cazorla alitumia miaka miwili nje ya dimba kuanzia Oktoba, mwaka 2016, wakati alipokabiliwa na hatari ya kukatwa mguu kutokana na kupata maambukizi baada ya kufanyiwa upasuaji kwenye kifundo cha mguu.

Hata hivyo, alirudi Villarreal akitokea Arsenal na kucheza mechi 86 kwa kipindi cha misimu miwili iliyopita, na akaitwa tena kwenye kikosi cha Hispania, Juni, mwaka jana na ataendelea na maisha yake ya soka nchini Qatar.

"Tumefikia makubaliano na Santi Cazorla,"ujumbe wa kwenye Twitter ya Al Sadd ulisomeka.

"Atawasili hapa Doha haraka kwa ajili ya kukamilisha taratibu za kimkataba na kujiunga na timu yetu. Karibu Al Sadd, Santi!

"Tunakutakia kila la heri na kwamba tunaweza kutwaa mataji mengi tukiwa pamoja. Asante sana."

Xavi amesaini mkataba wa mwaka mmoja na Al Sadd mwezi huu, licha ya kuhusishwa na na-



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO AZIDI KUNG'ARA ULAYA

Mshambuliaji huyo Mreno ameweka rekodi mpya ya kufunga mabao 50 mapema zaidi…

**TURIN,** Italia

KOCHA wa Juventus, Maurizio Sarri, amempongeza Cristiano Ronaldo kwa kuonyesha bidii ya hali ya juu baada ya kuwa mchezaji wa kwanza kufikisha mabao 50 kwenye Serie A hapo Jumatatu usiku.

**Mshambuliaji huyo Mreno alifunga mabao mawili ndani ya dakika tatu katika mechi dhidi ya wapinzani wao, Lazio na kuiweka Juventus karibu na kutwaa taji la ligi hiyo kwa mara nyingine.**

Ronaldo alifunga bao la kwanza kwa penalti iliyoamuriwa kwa msaada wa VAR na baadaye kufunga lingine akimalizika pasi kutoka kwa Paulo Dybala na kuifanya Juve ipate ushindi wa magoli 2-1.

Mabao mawili aliyofunga katika mechi hiyo yalimfanya Ronaldo afikishe jumla ya magoli 51 ndani ya Serie A, lakini amekuwa mchezaji wa kwanza kufikisha idadi hiyo kwa muda mchache, huku akiwa amecheza mechi 61 za ligi hiyo.

Straika wa zamani wa AC Milan, Andriy Shevchenko, aliweka rekodi ya kufunga mabao 50 baada ya kucheza mechi 68, wakati Mbrazili Ronaldo alifikisha idadi ya mabao 50 baada ya kucheza michezo 70.

Sarri akimpongeza mchezaji huyo ambaye anauwezo na kipaji kikubwa baada ya filimbi ya mwisho kupigwa, na kusisitiza kiwango chake kinaendelea kuimarika.

"Wakati Cristiano anakuwa na harufu ya damu, anakuwa kwenye kiwango bora zaidi, anaimarika mapema kati ya mechi na mechi," kocha huyo wa zamani wa Chelsea aliiambia Sky Sport Italia.

"Sio tu alikuwa sawa kimwili, lakini kisaikolojia pia.

"Ni mchezaji ambaye anatumia nguvu katika kila mechi, lakini anarejea katika hali ya kawaida mapema na anakuwa katika kiwango cha juu kwenye akili pamoja na miguu yake."

Kwa kufunga mabao hayo mawili, Ronaldo pia amekuwa mchezaji wa kwanza kuweka rekodi ya kufikisha mabao 50 katika Ligi Kuu England, LaLiga na Serie A.

Nyota huyo sasa amefunga mabao 51 akiwa Italia magoli 84 kwenye Ligi Kuu England wakati alipokuwa anacheza LaLiga aliweka wavuni mabao 311.

"Kila siku kuweka rekodi ni jambo muhimu, lakini muhimu zaidi ni timu kupata ushindi," alisema Ronaldo.

Juventus ilifanikiwa kulipa kisasi baada ya kufungwa mara mbili na Lazio katika mechi zilizochezwa Desemba, mwaka jana ambapo moja ni ya Serie A na nyingine ya Kombe la FA Italia (Super Cup).

## ZISIKUPITE

### AKE AKARIBIA CITY

MANCHESTER City inakaribia kumsajili beki wa Bournemouth na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Nathan Ake, ambaye ana umri wa miaka 25. ***(Guardian)***

### UNITED NJIA PANDA

MANCHESTER United huenda ikakubali au ikakataa kutoa pauni milioni 80, ili kumsajili winga wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho (20). ***(Star)***

### CHELSEA, LEVERKUSEN WATETA

CHELSEA iko katika mazungumzo na Bayer Leverkusen ili kujadili dau la pauni milioni 70 kwa lengo la kumsajili, Kai Havertz, huku tayari klabu nyingine zilizokuwa zinawania saini ya Mjerumani huyo mwenye umri wa miaka 21 zikiwa zimejitoa. ***(Sky Sports)***

### GERRARD AITOSA BRISTOL

KOCHA wa Rangers, Steven Gerrard bado anatajwa kuwa chaguo la kwanza la Bristol City ingawa kuna taarifa kwamba kocha huyo amekacha ofa ya kujiunga na klabu hiyo. ***(Bristol Post)***

### BRISTOL YAMTAJA HUGHTON

KOCHA wa zamani wa Newcastle na Brighton, Chris Hughton (61), yuko katika mazungumzo na klabu ya Bristol City inayoshiriki Ligi ya Championship ili kuwa na kocha mpya wa klabu hiyo. ***(Mail)***

### CEBALLOS AITAKA ARSENAL

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Hispania, Dani Ceballos (23), amesema atakuwa na furaha akiona anarejea katika kikosi cha Arsenal msimu ujao baada ya kuisaidia The Gunners kutinga fainali ya Kombe la FA, kutokana na mkataba wake wa mkopo kumalizika. ***(Sky Sports)***

### OBLAK KUIKAMUA CHELSEA

CHELSEA italazimika kumlipa nyota wa kimataifa wa Slovenia, Jan Oblak pauni milioni 110 kama ilivyoandikwa katika mkataba wake ili kulazimisha mazungumzo ya kumsajili golikipa huyo wa Atletico Madrid ambaye ana umri wa miaka 27. ***(Goal)***

### OZIL AIKATAA FENERBAHCE

KIUNGO wa Arsenal, Mesut Ozil (31), amekacha mazungumzo na klabu ya Fenerbahce nchini Uturuki, ambayo ilionyesha nia ya kumsajili Mjerumani huyo. ***(Bild)***

### PUEL ANUKIA WATFORD

KOCHA wa zamani wa Southampton na Leicester, Claude Puel anakaribia kutangazwa kuwa kocha mpya wa Watford baada ya klabu hiyo maarufu Hornets kumfukuza Nigel Pearson. ***(Mirror)***

### ANGUISSA ATAKIWA FULHAM

FULHAM inajiandaa kuwasilisha ofa ya pauni milioni 22.5 kwa klabu ya La Liga, Villarreal ili kumnasa kiungo, Andre-Frank Zambo Anguissa. Nyota huyo kutoka Cameroon msimu huu alikuwa anaitumikia Villarreal kwa mkopo. ***(Sky Sports)***

### MIN-JAE ANUKIA SPURS

LICHA ya kukataa ofa mbili, Tottenham inaamini itakamilisha mchakato wa kumsajili beki wa Beijing Guoan na Timu ya Taifa ya Korea Kusini, Kim Min-jae. ***(90min)***

HABARI MICHEZO

## Bigirimana kuiwahi Simba fainali FA

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI tegemeo wa Namungo FC, Blaise Bigirimana, anatarajiwa kuwapo katika kikosi kitakachoikabili Simba kwenye mechi ya fainali ya Kombe la FA, itakayochezwa Agosti 2, mwaka huu kwenye Uwanja wa Nelson Mandela, mjini Sumbawanga.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Namungo FC, Thiery Hitimana, alisema Bigirimana anaendelea vema na ana nafasi ya kumtumia katika mchezo huo wa kufunga pazia la msimu huu.

Hitimana alisema hali ya Bigirimana imeimarika na ataanza kumtumia katika mechi mbili za mwisho za Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Katika mechi za mwisho za ligi tutacheza na Mbao pamoja na Alliance FC, hatuna cha kupoteza ila natumia mechi hizo kuiandaa timu yangu kukabiliana na Simba, tutahakikisha tutakuwa imara kwa ajili ya kutafuta ushindi," alisema Hitimana.

Kocha huyo alisema anawaheshimu Simba kwa sababu ni timu nzuri na yenye wachezaji wazuri, hivyo analazimika kukijenga imara kikosi chake ili watimize malengo.

"Nina mechi mbili mkononi, sio ngumu kama itakavyokuwa fainali, naifahamu Simba nimekutana nayo, pia juzi nimepata nafasi kuwaona walivyocheza na Alliance, natakiwa kujipanga katika fainali hiyo," alisema Hitimana.

## Parimatch yaahidi kusaidia michezo

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya kubashiri ya Parimatch imezindua rasmi kampeni ya 'Amsha Ndoto na Parimatch' ambayo kila mwezi itakuwa inaendesha droo maalum itakayowezesha timu shiriki kujipatia vifaa vya michezo kutoka katika kampuni hiyo, imefahamika.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana wakati wa hafla fupi ya kukabidhi msaada kwa vituo vya kulelea watoto yatima vya Makao, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Parimatch, Tumaini Maligana, alisema timu zinazohitaji kupatiwa vifaa hivyo vitatakiwa kujiandikisha kupitia tovuti yao ya https://pma.bet/amshandoto.

Maligana alisema kila mwezi kampuni hiyo itakuwa ikichagua timu tano zitakazopatiwa vifaa, ikiwamo jezi, viatu, mipira na bibs huku malengo yao kwa mwezi ni kugawa vifaa mbalimbali kwa timu 60 jambo ambalo litasaidia katika kukuza sekta ya michezo.

"Timu zitatakiwa kujaza kikamilifu fomu za ushiriki na kuweka viambatanisho husika, tunaamini timu nyingi zitajitokeza ili zifaidike na vifaa tutakavyokabidhi," Maligana alisema.

Mkurugenzi huyo aliongeza kuwa kampuni yao inaendesha shughuli za kubashiri matokeo ya michezo kitaifa na kimataifa na kwa sasa wanafanya kazi kwenye nchi 15 duniani na wadau zaidi ya milioni moja wanashiriki. Katika hafla hiyo, Parimatch ilitoa msaada kwa vituo viwili ni Huruma Islamic pamoja na Amani Foundation vya jijini.

# MASHABIKI TAIFA STARS WAIANGUKIA SERENGETI

**Na Mwandishi Wetu**

MAFANIKIO ya Timu ya Taifa (Taifa Stars), yamewakuna mashabiki wa soka nchini, jambo ambalo limewafanya kutochelewa kuishukuru Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), kwa udhamini mnono wa miaka mitatu ulioiwezesha timu hiyo kufanya vizuri katika michuano mbalimbali ya kimataifa.

**Mashabiki hao wakiwamo wachezaji wa zamani waliochezea Taifa Stars, wameomba udhamini huo uendelee ili kuiwezesha Taifa Stars kupiga hatua zaidi na kuiweka nchi kwenye nafasi nzuri katika medani ya soka.**

SBL kupitia Bia ya Serengeti ilikuwa mdhamini mkuu wa Stars kuanzia mwaka 2017 baada ya kusaini mkataba wa miaka mitatu na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF).

Mmoja wa mashabiki ambaye ni mchezaji wa zamani wa Taifa Stars na mchambuzi wa soko nchini, Ally Mayai, alisema udhamini wa Serengeti ni mkubwa na wa kutia moyo na kuongeza kuwa umeichangia kuliweka soka la Tanzania katika nafasi nzuri.

"Udhamini huu umehusisha kiasi kikubwa cha fedha na tumeona matokeo yake kupitia kupanda kwa viwango vyetu katika Shirikisho la Soka Ulimwenguni (Fifa). Tuna kila sababu ya kuishukuru Kampuni ya Bia ya Serengeti," alisema Mayai, ambaye aliwahi kuwa nahodha wa Stars kati ya mwaka 1996 na 2004.

Shabiki mwingine na mchezaji wa zamani wa Stars, Mohamed Hussein 'Mmachinga' alisema udhamini wa Serengeti umeifanya Tanzania kupiga hatua kubwa kwenye miaka ya hivi karibuni.

"Ni katika kipindi hiki cha udhamini wa Serengeti tumeona timu yetu ikifuzu kushiriki mashindano makubwa ya Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon), Mashindano ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), kufuzu kwa Kombe la Dunia katika hatua ya makundi na kadhalika. Naamini mafanikio haya yataisukuma Serengeti kuendelea kuidhamini Stars," alisema Mmachinga.

Samson Kivuyo wa jijini Arusha alisema wakati udhamini mwingine ukilenga zaidi kuwavutia mashabiki kwenye bidhaa ya mdhamini, udhamini wa Stars umekuwa tofauti.

"Tumeshuhudia SBL ikihamasisha mashabiki na taifa kwa ujumla kupitia mabango, redio, televisheni na magazeti.

Hii imekuwa ikiwapa wachezaji morali ya kufanya vizuri kwa kuwa wanaona kama taifa tupo nyuma yao," alieleza.

Naye Hassanal Ochen wa Mikocheni jijini, Dar es Salaam alisema kwa udhamini wa SBL anaamini Tanzania miaka michache ijayo itakuwa ni mojawapo kati ya vigogo vya soka Afrika na duniani kwa ujumla.



Beki wa Simba, Shomari Kapombe (kushoto), akipambana kuwania mpira dhidi ya nyota wa Alliance FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, iliyochezwa Jumapili iliyopita kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Dodoma Jiji FC mipango itatimia

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA wa Ligi Daraja la Kwanza, Dodoma FC, wamesema hawatafanya mabadiliko makubwa katika kikosi chao ikiwamo benchi la ufundi linaloongozwa na Kocha Mkuu, Mbwana Makata kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara, imeelezwa.

Mwenyekiti wa Chama cha Soka Dodoma (DOREFA), Mulamu Ng'ambi, aliiambia gazeti hili watasajili wachezaji wachache wapya kwa kuzingatia maeneo ambayo wamebaini yana upungufu kwa kuongeza wachezaji wenye uzoefu.

Ng'ambi alisema moja ya makosa ambayo timu nyingi zinazopanda daraja na kucheza Ligi Kuu ni kukibadilisha kikosi karibuni chote kilichopanda na kusajili wachezaji wengi ambao wanaowaona ni wazoefu, lakini kutimua makocha waliozipandisha timu hizo.

"Katika kujenga timu ni lazima uwe na viti viwili au vitatu. Uwe na timu ya msingi ambayo umepanda nayo, halafu baadaye ndiyo kuangalia aina gani ya wachezaji ambao wanaweza kuboresha timu iliyopo ili iweze kushindana, lakini kwa sasa haipo hivyo, mpira umebadilika sana," alisema kiongozi huyo.

Mwenyekiti huyo Makata ni kocha anayeamini kuwajenga wachezaji vijana ambao ametoka nao chini na hajatofautiana na Juma Mgunda wa Coastal Union ambaye idadi kubwa ya wachezaji alionao ni wale walioipandisha timu hiyo.

"Changamoto imekuwa ni tabia ya viongozi kutowaamini walimu ambao wanapandisha timu, wao anaona viwango vyao ni vya kupandisha tu na baada ya hapo wanawaacha," alisema.

Jumamosi iliyopita, Dodoma FC ilitwaa ubingwa wa Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara baada ya kuifunga Gwambina FC bao 1-0 katika mechi ya fainali iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini, Dar es Salaam.

Michezo
Jumatano Julai 22, 2020
Nipashe



Ronaldo azidi kung'ara Ulaya UKURASA 22




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, akizungumza katika utambulisho wa mbio za hisani za "CRDB Bank Marathon" zilizoandaliwa kuhamasisha uchangiaji wa fedha kwa ajili ya upasuaji kwa watoto wenye magonjwa ya moyo katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI). Wengine pichani kutoka kulia Mkurugenzi Mkuu wa Strateguis, Kain Mbaya, Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Prof. Mohamed Janabi, Mkurugenzi Mtendaji wa Sanlam Insurance, Khamisi Suleiman, Mkurugenzi Mkuu wa Alliance Insurance, Byford Mutimusakwa na Ofisa Mkuu wa Fedha Benki ya CRDB, Fredrick Nshekanabo. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# YANGA: BIFU BENCHI LA UFUNDI LIPO HAPA

## ●●● Ni wakati ikiivaa Mtibwa leo, yaeleza sababu Mkwasa, Manyika kumwachia timu Eymael...

**Na Isaac Kijoti,** MOROGORO

WAKATI Yanga imewasili mjini hapa tangu juzi usiku tayari kwa mchezo wao wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Mtibwa Sugar utakaopigwa katika Uwanja wa Jamhuri leo, uongozi wa klabu hiyo umetolea ufafanuzi wingu zito lililotanda kuhusu benchi la ufundi la timu hiyo kudaiwa kugawanyika vipande viwili.

**Juzi Yanga iliwasili mjini hapa ikiwa na kikosi cha wachezaji 21, viongozi 10 huku benchi la ufundi likiongozwa na Kocha Mkuu, Mbelgiji Luc Eymael bila msaidizi wake, Boniface Mkwasa na Kocha wa Makipa, Manyika Peter, jambo ambalo baadhi ya mitandao ya kijamii na vyombo vya habari (si Nipashe) vimekuwa vikidai Eymael hawataki wasaidizi hao.**

Hata hivyo, Nipashe ambalo limetanda kila kona nchini ikiwamo mjini hapa, limemtafuta Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, ambaye ameongozana na timu hiyo na kutaka kujua ukweli kuhusu sintofahamu hiyo.

Alipoulizwa Bumbuli, alisema kutofautiana kupo kwa kila binadamu, na ni jambo la kawaida, lakini hakuna utata mkubwa katika benchi hilo la ufundi kama ambavyo unakuzwa na vyombo vya habari kwa baadhi kudai Eymael amewakataa wasaidizi wake hao.

Bumbuli alisema utata wa makocha hao ulianzia mazoezini juzi baada ya Mkwasa na Manyika kumweleza Eymael kwamba wanaomba wasiongozane na timu kutokana na kupata dharura, lakini kama inavyoeleweka Mbelgiji huyo mara nyingine 'hupaniki' na hivyo walianza kuvutana kabla ya yeye (Bumbuli) kuwataka wakayazungumzie hotelini.

"Baada ya kufika hotelini tuliwataka kila mmoja kueleza tatizo lipo wapi, ndipo Mkwasa akasema alimwomba abaki Dar es Salaam kwa sababu zake za kiafya kutokana na kusafiri sana, hivyo alitaka kupumzika akapate vipimo, na Manyika alieleza kuwa yeye hakuwa tayari kusafiri kwa sababu mkewe amefiwa na ndugu yake, hivyo alihitaji kwenda kuzika," Bumbuli alifafanua.

Si Mkwasa wala Manyika aliyekuwa tayari kupokea simu jana Nipashe ilipowatafuta kuzungumzia sakata hilo.

Kuhusu mazoezi ya jana yaliyofanyika katika Uwanja wa Jamhuri, yaliongozwa na Eymael akisaidiana na Kocha wa timu ya vijana, Said Maulid 'SMG'.

Akizungumzia mechi ya leo, Eymael alisema ana matumaini makubwa ya kufanya vizuri na kuiwezesha Yanga kumaliza katika nafasi ya pili kweye msimamo wa ligi hiyo ambayo tayari Simba imetwaa ubingwa kwa mara ya tatu mfululizo.

"Haitakuwa rahisi kwani Mtibwa Sugar iliyopo nafasi ya 14 kwenye msimamo ikiwa na alama 41 sawa na Lipuli, Mwadui na Alliance, inahitaji ushindi ili kujiweka katika nafasi nzuri zaidi ya kukwepa kushuka daraja ama kucheza mechi za mchujo," Eymael alisema.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, amesema anaamini mchezo huo utakuwa na ushindani mkubwa huku wakihitaji kushinda kutokana na nafasi waliyopo kwa sasa.

Katwila alisema huu umekuwa msimu mgumu, kutokana na matokeo ambayo hayaridhishi, lakini amekipanga kikosi chake kuhakikisha kinapata matokeo mazuri katika mchezo huo

## CRDB Marathon kukusanya milioni 200/-

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika mbio za CRDB Marathon zitakazofanyika Agosti 16, mwaka huu jijini Dar es Salaam kwa lengo la kukusanya fedha za kugharamia watoto wenye kuhitaji upasuaji wa moyo hapa nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela katika mbio hizo wanalenga kukusanga Sh. milioni 200 ili kusaidia gharama za matibabu kwa watoto 100 ambao wanasumbuliwa na ugonjwa huo.

Nsekela aliwataja viongozi wengine watakaoshiriki mbio hizo ni pamoja na Rais mstaafu Jakaya Kikwete pamoja na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harisson Mwakyembe.

"Kauli mbiu yetu katika mbio hizi za hisani ni 'Kasi Isambazayo Tabasamu', ikihamasisha watu wengi zaidi kujitokeza kushiriki kuleta tumaini la maisha na kusambaza tabasamu kwa watoto wenye magonjwa ya moyo," alisema Nsekela.

## Coastal Union yaipania Simba

**Na Somoe Ng'itu**

KOCHA Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda, amesema mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Simba haitakuwa nyepesi kwa sababu kila timu inahitaji kumaliza msimu wa 2019/20 kwa heshima.

Mgunda aliliambia gazeti hili kuwa, Coastal Union inahitaji 'kulipiza kisasi' cha mchezo wa mzunguko wa kwanza na itaingia uwanjani ikiwa haina presha.

"Utakuwa mchezo wa burudani lakini wenye malengo, hatutakubali kupoteza mchezo kirahisi, ingawa wote hatutakuwa na presha ya nje, tuko mahali salama na wenzetu (Simba), wameshachukua ubingwa," alisema kocha huyo.

Baada ya mechi hiyo, Simba itasafiri kuelekea Moshi, Kilimanjaro kuwafuata wenyeji Polisi Tanzania kwa ajili ya mchezo wa kufunga pazia la ligi utakaochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Chuo cha Ushirika.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >